# UPIMAJI WA UELEWA WA MATUMIZI YA MOFU NAFSI NA NJEO ZA KISWAHILI KWA WANAFUNZI WA SEKONDARI: MIFANO KUTOKA ZANZIBAR

**AZIZA MASOUD ADI**

**TASNIFU ILIYOWASILISHWA IKIWA NI SEHEMU YA MASHARTI YA KUTUNUKIWA SHAHADA YA UZAMILI (M.A. KISWAHILI - ISIMU) YA CHUO KIKUU HURIA CHA TANZANIA**

**2018**

## UTHIBITISHO

Aliyetia sahini hapo chini anathibitisha kuwa ameisoma na kuiangalia tasnifu hii inayoitwa: **‘Upimaji wa Uelewa wa Matumizi ya Mofu Nafsi na Njeo za Kiswahili kwa Wanafunzi wa Zanzibar”,** na napendekeza ikubaliwe na Chuo Kikuu Huria cha Tanzania, kwa minajili ya kukamilisha masharti ya kutunukiwa Shahada ya Uzamili ya Kiswahili (Isimu) ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

**……………………………………**

**Dkt. ZELDA ELISIFA**

**(Msimamizi)**

**Tarehe ....................................**

## HAKIMILIKI

Tasnifu hii hairuhusiwi kuiga au kunakili kwa vyovyote vile, kama vile kuchukua sehemu ndogo ya kazi hii, kieletroniki, kurekodi, kurudufu au njia nyingine yoyote bila ya idhini na ridhaa ya mwandishi wa tasnifu hii au kwa niaba ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

# TAMKO

Mimi, **AZIZA MASOUD ADI,** ninathibitisha kuwa tasnifu hii ni kazi yangu binafsi na haijawahi kuwasilishwa katika chuo Kikuu kingine chochotekwa ajili ya kutunukiwa Shahada ya Uzamili au Shahada nyengine yoyote.

**…………………………….**

**Aziza Masoud Adi**

**Tarehe………………………….**

## TABARUKU

Kazi hii naitabaruku kwa familia yangu, mume wangu mpendwa Haidar Bakari, watoto wetu wapendwa, Ahmed, Thuwaiba, Fatma, Hajra, Abubakar,Masoud na wengine watakaofuata wote nawambia iwe ni hamasa kwao, na wajitahidi kutafuta elimu kwa bidii na juhudi zote, kwani Elimu ni chachu ya  maisha bora.

## SHUKURANI

Kwanza natanguliza shukurani zangu za dhati kumshukuru Mwenyezi Mungu, mmiliki wa viumbe vyote vilioko baina ya Mbingu na Ardhi kwa kunijaalia uhai, uzima na uwezo wa kufanya utafiti na kuweza kuikamilisha kazi hii kwa kuandika matokeo ya utafiti, nikweli bila ya msaada wa Allah jambo lolote haliwezikusimama.

Vile vile niwashukuruwote walioniunga mkono kwenye kazi hii,kwa namna yoyote ile ambayo imeniwezesha kukamilisha kwa utafiti huu. Si rahisi kuwaorodhesha wote waliotoa mchango wao katikakufanikisha kazi hii, bali nawashukuru wote nitakaowataja na nisiowataja kwa mchango wao wa kufanikisha utafiti huu, nao wafahamu kwamba wameshiriki kwenye kazi hii.

Shukrani zangu mwanzo kabisa zimwendee msimamizi wa kazi hii Dr. Zelda Elisifa Sam, kwa kukubali kuwa msimamizi wangu, namshukuru kutokana na juhudi na ujasiri wake na ukomavu alionao kwangu mwanzoni mwa chimbuko la kazi hii yaani hatua ya kuandika pendekezo la utafiti mpaka pale kazi hii kukamilika kwake, naelewa wazi kuwa amenivumiliasana juu ya mapungufu yangu kama mwanafunzi, kwangu alikuwa muongozaji na mshauri mwelekezi,ni mwalimu mahiri na makini kwenye kazi anayoisimamia, alikubali kukaa nami kwa kunielekeza kwa sauti yenye hekimana upendo pale alipokuwa akinikosoa na kunielekeza,namuomba Mwenyezi Mungu amzidishie upendo na busara ili wajao nao wavune busara zake.

Haitokuwa vyema nisipotoa shukurani zangu za dhati kwa uongozi mzima wa Chuo Kikuu Huria cha Tanzania hasa Kitivo cha Sanaa na Sayansi ya jamii, mashirikiano

mwanana walionipatia na kuniwezesha kufanikisha kwa utafiti huu,Mungu awape maisha mema.

Shukurani zangu maalum ziwaendee wazazi wangu wapendwa, Baba Masoud Adi Amour na mama yangu Mrasha Ali Hemed, kwa mapenzi na haiba ya hali ya juu walionilea na kunitunza kwa kuniengaenga, kwani kumeniwezesha kusoma hadi kiwango cha elimu ya chuo Kikuu.

Nitakuwa mnyimiwa fadhila na shukurani pindi nikiacha kumshukuru mume wangu mpendwa Haidar Bakari na watoto wangu wotewapenzi, kwa kuweka uaminifu na ustahamilivu mkubwa kwamuda wote niliokuwa katika harakati za kufanya utafiti huu, walikuwa katika hali nzito na ngumu katika mfumo mzima wa maisha yao.

Sitoweza kuwasahau walimu na wanafunzi wote ambao nilikuwa nao bega kwa bega katika kufanikisha kazi hii. Kwa kuhitimisha, nawashukuru niliowataja na nisiowataja wote nawambia ahsanteni sana Mungu awaoengezeni ari, kasi na moyo wa kuwasaidia wengine.

## IKISIRI

Tasnifu hii ni matokeo ya utafiti uliolenga kuchunguza "upimaji wa uelewa wa matumizi ya mofu nafsi na njeo za Kiswahili kwa wanafunzi wa :mifano kutoka Zanzibar". Utafiti uliofanywa uliongozwa na malengo makuu mawili ambayo ni; Kuainisha kiwango cha uelewa wa maumbo ya mofu nafsi na njeo katika Kiswahili Sanifu kwa wanafunzi wa Zanzibar, na Kubainisha changamoto za ujifunzaji na ufundishaji wa mofu nafsi na njeo za Kiswahili Sanifu katika shule za Zanzibar.Mbinu zilizotumika katika ukusanyaji wa data ni pamoja na usaili kwa walimu na hojaji kwa wanafunzi, pia mtafiti alitumia mbinu ya maktabani katika maandiko mbalimbali ili kupata data za upili.Mbinu hizi zilichangia mtafiti kujua kiwango cha uelewa wa wanafunzi katika matumizi ya maumbo ya mofu nafsi na njeo katika Kiswahili Sanifu pamoja na changamoto zake. Nadharia zilizotumika katika uchambuzi wa data za utafiti huu ni nadharia ya mofofonolojia na nadharia ya Linganuzi. Sampuli iliyotumika katika utafiti huu, ni ya walimu 24 (30%) na wanafunzi 56 (70%), ambao kwa ujumla ni sawa  na watafitiwa 80 (100%). Matokeoya utafiti yanaonesha kwamba wanafunzi wanauwelewa wa 56.25% katika uchambuzi mofu nafsi na wastani wa 52.08% kwenyeuchambuzi wa mofu njeo. Utafiti ulibaini kuwa changamoto kubwa inayowakabili walimu na wanafunzi ni suala la uhaba wa vitabu rejea kwa walimu na hata wanafunzi wakati wa kujifunza mada hii. Kutokana na matokeo haya, utafiti huu unashauri mambo yafuatayo; kwanzawanafunzi kushirikishwa katika vitendo zaidi kuliko kufundishwa au kujifunza kwa nadharia.Pia Taasisi husika iengeze vitabu rejea vyakutosha vinavyohusiana na mada ya mofu. Halikadhalika wadau wa elimu wawe na uhusiano wa kutosha na walimu katika kuhamasisha ujifunzaji wa mada ya mofu kwa kutoa vipeperushi pamoja na kuandaa na kuwasilisha warsha na makongamano yanavyoonesha uchambuzi na uchanganuzi wa maumbo ya mofu.

# YALIYOMO

UTHIBITISHO ........................................................................................... i

HAKIMILIKI ............................................................................................. ii

TAMKO. ................................................................................................. iii

TABARUKU ............................................................................................ iv

SHUKURANI ............................................................................................ v

IKISIRI.. ................................................................................................. vii

YALIYOMO ............................................................................................ viii

ORODHA YA MAJEDWALI ..................................................................... xii

ORODHA YA CHATI ............................................................................. xiii

ORODHA YA VIFUPISHO ...................................................................... xiv

**SURA YA KWANZA: UTANGULIZI .................................................... 1**

1.1 Usuli wa Tatizo ................................................................................ 1

1.2 Tamko la Utafiti ................................................................................ 6

1.3 Malengo ya utafiti ............................................................................. 8

1.3.1 Lengo kuu ....................................................................................... 8

1.3.2 Malengo Mahsusi ............................................................................ 8

1.3.3 Maswali ya Utafiti ........................................................................... 8

1.4 Umuhimu wa Utafiti ......................................................................... 9

1.5 Mawanda ya Utafiti ......................................................................... 10

1.6 Vikwanzo vya Utafiti ....................................................................... 10

1.7 Muhtasari wa Sura ........................................................................... 11

**SURA YA PILI: MAPITIO YA KAZI TANGULIZI NA KIUNZI CHA NADHARIA ... 12**

2.1 Utangulizi ... 12

2.2 Kazi Tangulizi Kuhusu MofuNafsi na Njeo za Kibantu ... 12

2.3 Kazi Tangulizi Kuhusu Mofu Nafsi na Njeo za Kiswahili ... 14

2.4 Uelewa wa Wanafunzi katika Vipengele ya Kiisimu ... 16

2.5 Pengo la Maarifa ... 19

2.6 Kiunzi cha Nadharia ... 19

2.6.1 Nadharia ya Mofofonolojia ... 20

2.6.2 Nadharia Linganuzi ... 21

2.7 Muhtasari wa Sura ... 22

**SURA YA TATU: MBINU ZA UTAFITI ... 23**

3.1 Utangulizi ... 23

3.2 Eneo la Utafiti ... 23

3.3 Kundi Lengwa ... 24

3.4 Sampuli na Usampulishaji ... 24

3.4.1 Sampuli ... 24

3.4.2 Usampulishaji ... 26

3.5 Mbinu za Ukusanyaji Data ... 26

3.5.1 Hojaji ... 27

3.5.2 Usaili ... 28

3.5.3 Mbinu ya Maktabani ... 29

3.6 Mbinu za Uchambuzi wa Data ... 29

3.7 Maadili ya Utafiti ... 30

3.8 Muhtasari wa Sura ... 31

**SURA YA NNE: UWASILISHAJI NA UCHAMBUZI WA DATA ... 32**

4.1 Utangulizi ... 32

4.2 Kiwango cha Uelewa wa Maumbo ya Mofu Nafsi na Njeo Katika Kiswahili Sanifu ... 33

4.2.1 Uwasilishaji wa Data ... 33

4.2.1.1 Njia ya Hojaji ... 33

4.2.1.2 Njia ya Usaili ... 34

4.2.1.2.1 Walimu Waliosomea Fani la Kiswahili na Kukifundisha ... 35

4.2.1.2.2 Uzoefu wa Kufundisha Somo la Kiswahili ... 36

4.2.2 Kiwango cha Uwelewa waUchambuzi wa Maumbo ya Mofu ... 37

4.2.2.1 Kiwango cha Uwelewa Katika Uchambuzi Mofu Nafsi na Njeo ... 37

4.2.2.2 Idadi ya Viambishi Vinavyowakilisha Mofu njeo Katika Kiswahili Sanifu ... 39

4.2.2.3 Idadi ya Viambishi Vinavyowakilisha Mofu Nafsi katika Kiswahili Sanifu ... 40

4.2.2.4 Dhana ya Mofu na Mofimu ... 42

4.2.2.5 Uchambuzi wa Maumbo ya Mofu Nafsi kwenye Vitenzi ... 43

4.2.2.6 Uchambuzi wa Mofu Njeo Kwanye Vitenzi ... 46

4.3 Changamoto za Ujifunzaji na Ufundishaji wa Mada ya Mofu ... 50

4.3.1 Uwasilishaji wa Data ... 50

4.3.1.1 Walimu Waliopatiwa Muongozo/Mafunzo ya Mada ya Mofu ... 51

4.3.1.2 Aina za Miongozo/Mafunzo Katika Kufundisha Mada ya Mofu ............... 52

4.3 Changamoto Katika Kujifunza na Kufundisha Mada ya Mofu .................. 53

4.3.3.1 Changamoto Katika Ufundishaji wa Mada ya Mofu kwa walimu.............. 54

4.3.2.2 Changamoto Katika Kujifunza Mofu Nafsi na Njeo kwa wanafunzi......... 60

4.4 Muhtasari wa Sura ........................................................................... 64

**SURA YA TANO MUHUTASARI WA UTAFITI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO........................................................................................ 66**

5.1 Muhutasari wa Utafiti ...................................................................... 66

5.2 Muhtasari wa Matokeo ya Utafiti ............................................................. 67

5.3 Hitimisho.................................................................................................. 68

5.4 Mapendekezo ya Utafiti ................................................................................ 69

5.4.1 Mapendekezo kwa Tafiti Fuatishi................................................................ 69

5.4.2 Mapendekezo kwa Wadau wa Elimu.......................................................... 70

**MAREJELEO ........................................................................................... 71**

**VIAMBATISHO ......................................................................................... 77**

## ORODHA YA MAJEDWALI


Jedwali Na 1.1 Viambishi Tamati vya Philipino (Philipine Suffixes) .................... 2

Jedwali Na.3.1 Sampuli ya Watafitiwa ................................................................ 25

Jedwali Na. 4.1 Viwango vya Elimu, Jinsia na Shule Walizotokea Wahojiwa ..... 34

Jedwali Na.4.2 Walimu Waliosomea Fani ya Kiswahili na Kukifundisha ........... 35

Jedwali Na.4.3 Uwezo wa Wanafunzi wa Kuchambua Maumbo ya Mofu Nafsi na Njeo Wakati wa Kufundisha .......................................... 38

Jedwali Na. 4.4 Uwelewa wa Viambishi VinavyowakilishaMofu Njeo ............... 39

Jedwali Na. 4.5 Uwelewa wa Viambishi VinavyowakilishaMofu Nafsi ............... 41

Jedwali Na. 4.6 Uchambuzi wa Mofu Nafsi Kwenye Vitenzi ............................... 44

Jedwali Na. 4.7 Uchambuzi wa Mofu Njeo Kwenye Vitenzi ................................ 47

Jedwali Na. 4.8 Walimu Waliopatiwa Muongozo / Mafunzo ya Mada ya Mofu ......................................................................................... 51

Jedwali Na.4.9 Changamoto za Ufundishaji wa Mofu Nafsi na Njeo .................. 54

Jedwali Na.4.10 Changamoto za Ujifunzaji kwa Wanafunzi ................................. 59

## ORODHA YA CHATI

Chati Na.4.1 Uzoefu wa ufundisha somo la Kiswahili .......................................... 36

Chati Na.4.2 Aina za Miongozo/Mafunzo Katika Ufundishaji Mada ya Mofu .... 52

## ORODHA YA VIFUPISHO

| | |
|---|---|
| BLMT | Baraza la Mitihani Tanzania |
| CD | Compact Disc |
| DVD | Digital Vedeo Disc |
| Kesh | Keshatajwa |
| Na. | Namba |
| N.D | Not indicated |
| n.k | Nakadhalika |
| N1 | Nafsi ya kwanza |
| N2 | Nafsi ya pili |
| N3 | Nafsi ya tatu |
| SPSS | Software Package for Statistical Sciences |
| U | Umoja |
| W | Wingi |
| ZMRC | Zanzibar Madrasa Resource Centere |
| Ø | Kapa |

# SURA YA KWANZA

# UTANGULIZI

## 1.1 Usuli wa Tatizo

Kila lugha ina miundo na kanuni zake ambazo hutofautiana na nyengine kutokana na maeneo pamoja na mpangilio wa matamshi. Nyanja ya mofolojia ndiyo inayoshughulikia maumbo ya maneno ambayo hujengwa na mofu mbalimbali ili kukamilika kwa neno. Dhana ya mofu kama ilivyofasiliwa na Massamba (2004) alienukuliwa na Matinde (2012) anaeleza kwamba mofu ni kipashio cha kimaumbo ambacho huwakilisha mofimu, anaendelea kusema kwamba mofu ni umbo kamili ambalo huwakilisha mofimu na hudhihirika kifonolojia na kiothografia.

Suali la mofu na mofimu limechambuliwa katika lugha mbalimbali ulimwenguni, kwa kuangaliwa na wataalamu kutoka nchi tofauti, baadhi yao ni Mrayat (2015) ambaye alichunguza mofimu za ukanushi katika lugha ya Kiarabu (Jordan), na akagundua kuwa wazungumzaji wa mjini na vijijini katika lugha ya Jordan wanatumia ukanushi (- miʃ) kabla ya neno, mfano neno “zain” (nzuri) miʃzain (sio nzuri). Wakati wazungumzaji wa vijijini wanaongeza (mo) kabla ya neno mfano mozain (sio nzuri), pia mabedui wanaongeza (mahob) mfano mahobzain (sio nzuri).

Aswan na wenzake (2015), waliangalia ufahamu wa elimu ya mofimu kwa vijana katika kujifunza maneno mapya Malaysia. Watafiti hawa waligundua kwamba vijana wanaojifunza wanaufahamu wa kawaida kwa kutumia muundo wa mofolojia katika maneno. Watafiti hawa walishauri kwamba kuwe na maelekezo ya wazi katika mofolojia ambayo inaweza kutumika kama ni mikakati katika kuendeleza ujuzi wa mofimu miongoni mwa vijana wanaojifunza katika Malaysia.

Mtaalamu Khan (2014) alichambua juu ya  uwasilishaji wa mofimu katika vitabu nchini Pakistan, na alibaini kwamba mofimu huru (single morpheme) 90% ziko sawa. Pia mpangilio wa Sarufi hauna athari katika mpangilio wa upatikanaji wa mofimu, lakini unaathiri asilimia ya upatikanaji wa mofimu kuwa ni mdogo.

Aidha Pedroza (N.D) aliangalia tafiti nyingi zilizofanywa katika nchi yakeya Philipinojuu yauchambuzi wa mofu, baadhi ya tafiti zilifanywa kwa muktadha wa kutoa makisio ya matumuzi ya lugha. Tafiti hizi ziliangalia juu ya uchambuzi wa mofu za Kiphilipino ambazo ziliunda na kuathiri mizizi ya neno.Matokeo ya tafiti hizi yaliweka wazi kuwa athari za mofu za kiphilipino katika mizizi yaliwekwa kwa utaratibu uliohusishwa katika matumizi, pia tafiti zilitoa hati kwa wapenda sanaa. Zaidi ya hayo tafiti hizi zilitoa ufahamu mzuri katika herufi za lugha za Kifilipino.

**Jedwali Na 1.1 Viambishi Tamati vya Philipino (Philipine Suffixes)**

| **Maneno ya Kiphilipino** | **Tafsiri kwa Kiingereza** | **Viambishi Tamati** | **Mzizi wa Maneno** | **Tafsiri kwa Kiingereza** |
|---|---|---|---|---|
| Iyak-in | Cry-baby | In | Iyak | Cry |
| Hati-an | To share | An | Hat | Devide, spit |

Hapa inaonekana kwamba viambishi vinatofautiana katika matumizi, kiambishi tamati “in” kinapokuwa mwisho kinakuwa kiambishi cha sifa mfano iyakin. Kwa upande mwengine kiambishi “an” kinakuwa kitenzi mfano hatian.

Mtavangu (2008) ambae alishughulika na njeo zilizokuemo katika lugha ya Kihehe, na alibaini kuwa lugha ya Kihehe haina mofu maalum ila hudhihirishwa na sauti katika wakati uliopita muda mfupi na wakati ujao, mfano wakati uliopita muda

mfupi: A – tof – i’le – umwana- (amempiga mtoto), pia alionesha njeo za wakati ujao mfano

mu- o- pya (utachomwa).

Hamadi (2011) aliangalia viambishi njeo na hali mbalimbali kati ya Kipemba na Kiswahili sanifu, katika uchunguzi wakealibaini kwamba viambishi vya Kiswahili Sanifu vinaachana na viambishi vya Kipemba kwa kiasi kikubwa.

Kwahivyo mtafiti anaona kwamba swali la mofu na mofimu ni muhimu sana katika lugha kwani ni viambajengo vikuu katika neno.

Katika uchambuzi wa isimu ya lugha ya Kiswahili, mofu imejengwa na viambishi mbalimbali kama vile nafsi, njeo, tamati n.k. Mofu nafsi huonesha nafsi ya msemaji na nafsi inayozungumzwa ambayo ni ya umoja au wingi, wakati mofu njeo huonesha wakati au hali ya kutendeka kwa kitendo (Matinde, 2002). Haya yanathibitishwa katika mfano wa neno **a-na-**cheza, katika neno hili–{a} inawakilisha nafsi ya tatu umoja, na –{na} inawakilisha njeo ya wakati unaoendelea. Katika lugha ya Kiiengereza njeo haziwezi kusimama peke yake na kuleta maana ila nafsi zina uwezo wa kusimama pekeyake mfano *he write* – anaandika, *you wrote* - uliandika. ukiangalia mifano hii tulibaini kuwa–{he} imesimama peke yake ambayo ni nafsi ya tatu umoja, na –{you} ni nafsi ya pili umoja au wingi,–{i} ni ilioungana na neno ni njeo ya wakati unaoendelea na –{o}wakati uliopita. Mtaalamu Faynan (1998) alifafanua mofu nafsi na njeo za Kiarabu katika maneno **ka**tab**ta** – *uliandika*, **ka**tabtu**m** – *muliandika*, **ya**ktubu – *anaandika* – **na**ktubu **-** *tunaandika*. Kutokana na maneno haya ilionekena wazi kwamba mofu nafsi na njeo za Kiarabu huegemezwa

kwenye kitenzi, kama inavyooneka –{ka} inawakilisha njeo za wakati uliopita, –{ya} na –{na} zinawakilisha wakati unaoendelea ambapo –{ta} ni nafsi ya pili umoja na –{ku} ni nafsi ya pili wingi.

Hassan (2016) alilinganisha mofu njeo na nafsi kati ya lahaja ya Kipemba na Kiswahili sanifu, na alichokiona nikuwa kuna tofauti kubwa ya ujidhihirishaji wa maumbo ya mofu kati ya Kiswahili Sanifu na Kipemba. Vilevile Barno (2013) moja kati ya vipengele alivyochunguza katika kazi yake ni njeo katika lugha ya Kinandi, na aligundua  kuna nyakati mbalimbali katika lugha ya Kinandi kama wakati uliopita, uliopo, na ujao kwa kutumia nadharia ya kanuni finyu ya Chomsky (1995 na 2000). Kwa mantiki hiyo ipo haja ya kupima uelewa wa wanafunzi juu ya maumbo ya mofu nafsi na njeo za Kiswahili.

Mbali ya Wanaisimu walioangalia swali la mofimu katika lugha mbalimbali, pia kuna baadhi ya wanaisimu walipima uwezo wa wanafunzi katika vipengele mbalimbali vya kiisimu, miongoni mwa wataalamu hao ni; Kitsao (2015) ambae alichunguza makosa ya kisarufi katika insha kwa wanafunzi wa shule za msingi ambayo yalichangia matokeo mabaya ya mitihani, kata ya Ganze, Kaundi ya Kilifi, Kenya. Katika utafiti wake aligundua kuwa baadhi ya wanafunzi kutokuwa wabunifu kwa kuandika wenyewe, kwa vile hurudia mifano waliopewa na walimu wakati wanapofundisha. Halikadhalika Nyagah (2016) naye alichunguza makosa ya kifonolojia na kimofolojia yaliyojitokeza katika kazi andishi za wanafunzi wa shule za upili, Tigania, jimbo la Meru, na alibaini kuwa makosa yaliyojitokeza kwenye insha za wanafunzi ni ya unazalishaji wa fonimu, udondoshaji wa sauti, uchopekaji wa irabu na utumiaji wa sauti mbadala. Vile vile Obara (2014) alichanganua makosa

yanayofanywa na wanafunzi wazungumzaji wa lugha ya Ekegusii,mtafiti huyu aligundua kuwa miongoni mwa makosa hayo yalitokana na baadhi ya walimu wa Ekegusii ambao wanautendaji mbaya katika uzungumzaji unaoathiri wanafunzi hao. Aidha Mathooko (2002) alichunguza matatizo yanayoikumba Kiswahili kama lugha ya kujifunzia isimu na vyuoni vikuu nchini Kenya, na alibaini kwamba asilimia kubwa ya wanafunzi wa lugha ya Kiswahili vyuoni hawafanyi vizuri katika somo la isimu ikilinganishwa na masomo mengine yanayofundishwa. Pia Mohammed (2010) alichunguza matatizo wanayoyapata wanafunzi wa Libya katika kujifunza viambishi vya njeo katika lugha ya Kiswahili. Kwa kiasi fulani utafiti wake ulibaini matatizo yaliyowakabili wanafunzi wa Libya wanaojifunza Kiswahili, na walimu wanaofundisha lugha hiyo, ili kuweza kuwasaidia hasa wanafunzi kumudu vizuri maswali ya kisarufi ya Kiswahili Sanifu wakati wanapojifunza.

Kiujumla baadhi ya orodha ya watafitiwa hao walichunguza mofimukwenye vipengele tofauti katika lugha mbalimbali, vilevile kuna wanaisimu wengine waliangalia makosa mbalimbali yaliyofanywa na wanafunzi katika vipengele mbalimbali vya kiisimu.

Mtafiti alilenga kuwapimawanafunzi juu ya matumizi ya mofu nafsi na njeo za Kiswahili sanifu, ambacho kilisanifiwa na kuteuliwa kutumika kuwani mawasiliano ya lugha za Kibantu, na Kiunguja mjini ndicho kilichoteuliwa kusanifiwa. Kiswahili kiliteuliwa kuwa lugha ya taifa 1964 ambapo katika shughuli zote za kitaifa ziliendeshwa kwa kutumia lugha ya Kiswahili. Hivyo Kiswahili kilihimizwa kutumika katika mawasiliano yote hususani katika shughuli za umma na wizara zote, serekali na Bunge, Kiswahili kiliendelea kupanda hadhi zaidi wakati wa Azimio la

Arusha la mwaka 1967, Azimio hilolilitungwa na kuandikwa kwa lugha ya Kiswahili (Kipacha, 2002).

Katika lugha yoyote ile lazima yawepo mawasiliano katika jamii husika, kama walivyo walimu na wanafunzi huwa na mawasiliano wawapo shuleni na hutumia Kiswahili Sanifu lakini bado hujitokeza changamoto mbalimbali katika matumizi ya maumbo ya mofu nafsi na na njeo kwa wanafunzi wao. Hivyo watafiti waliotangulia waliangalia matumizi ya mofimu katika lugha mbalimbali, na baadhi ya wataalamu walichunguza matatizo yanayowapata wanafunzi katika shule tofauti, lakini hawakupima uwelewa wa matumizi ya mofu nafsi na njeo. Kwa hivyo mtafiti ataziba pengo hili kwa kuainisha kiwango cha uelewa wa maumbo ya mofu nafsi na njeo katika Kiswahili kwa wanafunzi wa Zanzibar, pamoja na kubainisha changamoto za ujifunzaji na ufundishaji wa mofu nafsi na njeo za Kiswahili Sanifu katika shule za Zanzibar.

## 1.2 Tamko la Utafiti

Dhana ya mofofonolojia ni pana sana inayojumuisha matawi mawili ya kiisimu; tawi la mofolojia na tawi la fonolojia. Mjumuisho huu unaweza kujenga ugumu kwa mchambuzi wa mofofonolojia na vipengele vyake. Kwa hivyo, uelewa uchambuzi wa mofu unachuku11wa nafasi muhimu katika utambuzi wa lugha kiisimu.

Kuna wataalamu wengi waliogusia kuhusiana na mofu katika miktadha mbalimbali kwa mfano,Massamba (2004) alienukuliwa na Matinde (2012) anaeleza kwamba mofu ni kipashio cha kimaumbo ambacho huwakilisha mofimu. Wataalamu wengine waliofanyia tafiti juu ya mofimu ni pamoja naHassan (2016) ambaye alilinganisha

mofu njeo na nafsi kati ya lahaja ya Kipemba na Kiswahili sanifu. Vilevile Barno (2013) moja kati ya vipengele alivyochunguza katika kazi yake ni njeo katika lugha ya Kinandi.Halikadhalika Mohamed (2010) alitafiti matatizo wanayoyapata wanafunzi wa Libya katika kujifunza viambishi vya njeo katika lugha ya Kiswahili.

Mbali ya watafitiwa hao, pia kuna watafiti mbalimbali waliochunguza matatizo yanayowapata wanafunzi katika nyanja za kiisimua katika vipengele mbalimbali, baadhi yao ni Nyagah (2016) naye alichunguza makosa ya kifonolojia na kimofolojia yaliyojitokeza katika kazi andishi za wanafunzi wa shule za upili, Tigania, jimbo la Meru.Halikadhalika Kitsao (2015) ambae alichunguza makosa ya kisarufi katika insha kwa wanafunzi wa shule za msingi.Vile vile Obara (2014) alichanganua makosa yanayofanywa na wanafunzi wazungumzaji wa lugha ya Ekegusii. Aidha Mathooko (2002) alichunguza matatizo yanayoikumba Kiswahili kama lugha ya kujifunzia isimu na vyuoni vikuu nchini Kenya.

Kwa hivyo watafiti hawa wote waliangalia matatizo yanayowapata wanafunzi katika vipengele tofauti vya kiisimu, lakini hakujitokeza mtafiti hata mmoja kupima uwelewa wa maumbo ya mofu nafsi na njeo za Kiswahili kwa shule za Zanzibar. Kwa vile Zanzibar pia kuna shule za  na hakuna hata stadi moja ya maswali haya iliyofanyika Zanzibar, kwa hivyo ipo haja kubwa sana ya kuangalia eneo la Zanzibar kwani wanafunzi wanahitaji kuelewani kwa kiasi gani wanaweza kuainisha na kuchambua maumbo ya mofu nafsi na njeo za Kiswahili sanifu,  pamoja na kubaini changamoto za ujifunzaji mada ya mofu.

Hivyo mtafiti ataziba pengo hilo kwa kupima kiwango cha uwelewawa maumbo ya mofu nafsi na njeo za Kiswahili kwa wanafunzi wa Zanzibar katika uchambuzi wa vitenzi mbalimbali.Sambamba na hilo utafiti pia utajikita katika kubainisha changamoto mbalimbali za ujifunzaji na ufundishaji wa mofu nafsi na njeo katika shule za Zanzibar.

## 1.3 Malengo ya utafiti

Katika malengo ya utafiti kuna malengo makuu na malengo mahsusi.

### 1.3.1 Lengo kuu

Lengo kuu la utafiti huu ni kupima uelewa wamatumizi ya mofu nafsi na njeo katika Kiswahili kwa wanafunzi wa shule a Zanzibar.

### 1.3.2 Malengo Mahsusi

i. Kuainisha kiwango cha uelewa wa maumbo ya mofu nafsi na njeo katika Kiswahili Sanifu kwa wanafunzi wa Zanzibar.

ii. Kubainisha changamoto za ujifunzaji naufundishaji wa mofu nafsi na njeo za Kiswahili Sanifu katika shule za Zanzibar.

### 1.3.3 Maswali ya Utafiti

i. Ni kiwango gani cha uwelewa wa maumbo ya mofu nafsi na njeo katika Kiswahili Sanifu kwa wanafunzi wa Zanzibar?

ii. Kuna changamoto gani za ujifunzaji na ufundishaji wa mofu nafsi na njeo za Kiswahili Sanifu kwa wanafunzi wa shule za Zanzibar?

## 1.4 Umuhimu wa Utafiti

Baada ya kukamilika kwa utafiti huu, utawasidia watafiti wajao, walimu, pamoja na wanafunzi wangazi tofauti katika fani ya isimu kwa kubaini uwezo wa wanafunzi katika matumizi ya maumbo ya mofu nafsi na njeo za Kiswahili Sanifu.

Kwa kuwa utafiti huu ulibaini changamoto za ufundishaji na ujifunzaji wa mada ya mofu, kwahiyo utakuwa ni mwanga kwa walimu wanaofundisha somo la Kiswahili kwa kuelewa kama changamoto hizo hujitokeza wakati wa kufundisha. Piawalimuwalibaininjia mbali mbali za kuwasaidia wanafunzi wao katika ufundishaji wa mada ya mofu.

Halkadhalika utafiti huu utapanua mawanda ya utafiti kwa watafiti wengine katika kuendelezatafiti katika maeneo yanayohusiana na mofu katika lugha ya Kiswahili Sanifu na lugha nyingine.

Vilevile utafiti huu, utasaidia wadau pamoja na watunga sera ya elimu, kuelewa changamoto zinazojitokeza kwa walimu na wanafunzi kwa lengo la kufuatilia suala zima la ufundishaji na ujifunzaji wa mada ya mofu katika shule za Zanzibar.

Aidha utafiti huu utawasaidia wataalamuwa lugha ya Kiswahili kuonanamna gani wanaweza kukabiliana na matatizo hayo.

Pia utafiti huu utapanua mawanda ya utafiti kwa watafiti wengine katika kuendelezatafiti katika maeneo yanayohusiana na mofu katika lugha ya Kiswahili Sanifu na lugha nyingine.

## 1.5 Mawanda ya Utafiti

Utafiti huu ulichunguza uwelewa wa mofu nafsi na njeo za Kiswahili kwa wanafunzi wa shule za Zanzibar kwenye uwanja wa mofolojia. Katikakuchunguza kipengele hiki mtafiti aliangalia wanafunzi wa Zanzibar jinsi walivyoainisha na kuchambua maumbo ya mofunafsi na njeo za Kiswahili Sanifuwakati wa utafiti. Pia mtafiti aliangalia changamoto za ujifunzaji kwa wanafunzi na za ufundishaji kwa walimu wa Zanzibar.

Kazi hii haikujikita katika maumbo mengine ya mofu kama vile urejeshi, ukanushi, tamati nakadhalika. Maumbo ya mofu nafsi na njeo mtafiti aliamua kuyafanyia utafiti kwa kina kwasababu ndio viambajengo vya msingi katika maneno.

## 1.6 Vikwanzo vya Utafiti

Katika utafiti huu mtafiti alikabaliana na vikwanzo mbalimbali ambavyo vilimsababishia ugumu katika muendelezo mzima wa kazi yake, miongoni mwa vikwanzo hivyo vilitokana na mtafiti kuteua shule nne (4) tu kutoka katika mkoa wa mjini Magharibi, hali hii ilichukuliwa kama ni changamoto ya utafiti huu kwa kutoyapata matokeo ya shule zote za Zanzibar. Hivyoutafiti zaidi unahitajika katika mikoa mingine kwa lengo la kuona hali halisi ya changamoto za mada ya mofu kwa wanafunzi wa Zanzibar, pamoja na kutathmini kwa kiwango cha juu matumizi ya mofu nafsi na njeo kwa wanafunzi wa Zanzibar. Pia, changamoto nyengine ni zile zilizotokana na naadharia moja ya kitafiti ya mofofonolojiakushindwa kujitosheleza katika kazi hiikwa vile ilichunguza muundo wa mofimu katika lugha, nahaikuangalia matatizo katika kujifunza. Hivyo ili kuepukana na mapungufu ya nadharia ya

mofofofolojia, mtafiti aliengeza nadharia nyengine ya linganuzi ilikumuungozea mtafiti katika lengo la pili la utafiti wake.

## 1.7 Muhtasari wa Sura

Sura hii inaelezea utangulizi wa utafiti huu pamojana kufafanua vipengele mbalimbali ambavyo ni muhimu katika utafiti huu, vipengele hivyo ni pamoja na usuli wa mada ya utafiti, tamko la utafiti, lengo kuu la utafiti, malengo mahsusi, maswali ya utafiti, umuhimu wa utafiti, mawanda ya kitaaluma na mipaka yake, vikwazo vya utafiti na utatuzi wake pamoja na mpango wa utafiti. Sura inayofuata inazungumzia upitiaji wa maandiko na machapisho mbalimbali yanayohusiana na mada ya utafiti wetu.

# SURA YA PILI

# MAPITIO YA KAZI TANGULIZI NA KIUNZI CHA NADHARIA

## 2.1 Utangulizi

Katika sehemu hii mtafiti alipitia maandiko mbalimbaliyanayohusu isimu,kwakuangalia vipengele vya mofu nafsi na njeo, pia aliangalia changamoto wanazokumbana nazo wanafunzi katika vipengele mbalimbali vya kiisimu.

## 2.2 Kazi Tangulizi Kuhusu MofuNafsi na Njeo za Kibantu

Kuna baadhi ya wataalamu walifanya utafiti katika lugha za Kibantu kwa kuangalia mofu nafsi na njeo katika lugha mbalimbali. Miongoni mwao ni Mtavangu (2008) ambae alishughuliki njeo zilizokuwemo katika lugha ya Kihehe. Kazi yake ilitusaidia sana kwani tulielewa kwamba katika lugha ya Kihehe haina mofu maalum za wakati ujao na wakati uliopita muda mfupi, isipokuwa hudhihirishwa na sauti, mfano wakati uliopita muda mfupi:

A – vimb – i’te – yaliomo. (amelia)
A – tof – i’le – umwana. (amempiga mtoto)
Aidha Mtavangu (kesh ) pia alionesha njeo za wakati ujao, mfano;

Mu- o- pya (utachomwa).Mtafiti alionesha jinsi sauti ilivyojitokeza mwishoni mwa viambishi tamati. Kazi ya mtafiti huyu ilitusaidia sana katika utafiti wetu ingawa haikuangalia mofu nafsi inavyojitokeza katka lugha ya Kihehe.

Barno (2013) nae alichunguza muundo wa mofofonolojia ya kikundi kitenzi cha Kinandi.Moja kati ya vipengele alivyochunguza katika kazi yake ni njeo katika lugha ya Kinandi, na aligundua kuwa kuna nyakati mbalimbali katika lugha ya Kinandi kama wakati uliopita, uliopo, na ujao. Mfano:

| **Kinandi** | **Wakati** | **Kiswahili** |
|---|---|---|
| Atieni | wakati uliopo | ninaimba |
| Katieni | wakati uliopita | nilikuwa ninaimba |
| Tunatieni | wakati ujao | nitaimba |

Sambamba na hayo Barno (kesh) anaendelea kufafanua kuwa kuna wakati wa muda mrefu huoneshwa kwa kiambishi **ki**- wakati uliopita muda mrefu kiasi hubainishwa kwa **ko**-, na wakati uliopita muda mfupi huoneshwa kwa kibainishi **ka**-,pia kibainishi cha wakati uliopita wa mbali ni **ki**- na wakati ujao ni**tun**-

Mfano wa vibainishi vya njeo katika Kinandi ni hivi vifuatavyo:

[ki] - muda mrefu

[ko] - muda mrefu kiasi

[ka] - mfupi

[kitun] - muda mrefu sana wa nathari

Aliendelea kufafanua mofu nafsi katika lugha ya Kinandi, ambayo hutokea katika nafsi zote tatu. Mfano:

| | |
|---|---|
| anee (mimi) | N1U |
| acheck (sisi) | N1W |
| inyee (wewe) | N2W |
| okwele (nyinyi) | N2W |
| ince (yeye) | N3 U |
| icheck (wao | N3 W |

Kwa hivyo kazi ya mtafiti huyu ilitusaidia sana kuelewa njeo za wakati tofauti, ikiwa ni wakati uliopo, uliopita na wakati ujao.

## 2.3 Kazi Tangulizi Kuhusu Mofu Nafsi na Njeo za Kiswahili

Wataalamu kadhaa walichunguza maumbo ya nafsi na njeo katika Kiswahili, kati yao ni: Mazrui (1983) alichunguza tofauti za mofimu zinazowakilisha njeo kati ya lahaja ya Mvita, Bajuni, Amu, na Unguja, katika kazi yake mtafiti aligundua kuwepo tofauti za maumbo ya mofimu zinazowakilisha njeo katika lahaja alizozitumia, Hivyo katika utafiti wetu huu mbali ya kuangalia kipengele cha mofu njeo, pia tuliangalia na mofu nafsikwa kuwapima wanafunzi wa shule za Zanzibar, hali ambayo haikupata fursa ya kushughulikiwa na Mazrui katika kazi yake. Kazi ya Mazrui ilitoa mchango mzuri kwa kummurikia mtafiti katika kazi yake kutokana na mfanano na kazi zetukwa kuelewa nyakati mbalimbali katika lugha ya Kiswahili.

Aidha kuna baadhi ya wataalamu walichunguza maumbo ya nafsi katika kazi zao, na miongoni mwa hao ni:Nassor (2014)naye aliangalia na kujadili mifanyiko ya kimofolojia ya vitenzi vya lahaja ya Kimakunduchi Zanzibar, ambae aligusia pia na kipengele cha mofu nafsi, na alibaini kuwa vitenzi vya lahaja ya Kimakunduchi vina mifanyiko ya kimofolojia inayoweza kutambulishwa, na vitenzi vinavyotokea kabla ya mzizi (viambishi nafsi).Katika uchanganuzi wake ameonesha vimbishi vya nafsi katika hali zote sita katika lahaja ya kimakunduchi.

| | | |
|---|---|---|
| N1: | U ni (Ø) | W ni (tu) |
| N2: | U ni (ku) | W ni (m) |
| N3: | U ni (ka) | W ni (wa) |

Pia, Nassor (kesh) alichambua mifanyiko ya viambishi awali vya njeo, na aligundua viambishi vya njeo vilivyotumika katika vitenzi vya lahaja ya Kimakunduchi. Kwa mfano:

Wakati uliopita kitenzi huchukuwa kiambishi –{Ø}.
Wakati unaoendelea huchukuwa kiambishi -{ma}.
Wakati ujao huchukuwa kiambishi –{cha}.

kazi ya mtafiti huyu ilitunufaisha kwa upande wetu hasa katika uchanganuzi wake wa mofu nafsi na njeo, ambayo ndiyo muelekezo mzuri wa kazi yetu, kwa kuchambua vitenzi mbalimbali vya lugha ya KIswahili, ili kuweza kuwapima wanafunzi kuhusu matumizi ya mofu njeo na nafsi za Kiswahili.

Hassan (2016) naye alichambua juu ya udhihirishaji wa mofu zinazowakilisha nafsi na njeo katika Kiswahili Sanifu na lahaja ya Kipemba, na alibaini kwamba kuna tofauti kubwa ya ujidhihirishaji wa maumbo ya mofu kati ya Kiswahili Sanifu na Kipemba. Kazi ya Hassan (kesh) ilitusaidia sana kwa kutuelewesha aina za mofu za Kiswahili Sanifu wakati wa kupima uelewa wa wanafunzi katika mofu nafsi na njeo za Kiswahili sanifu.

Mohammed (2013) alijishughulishana uchunguzi waathari za kiisimu za lahaja ya Kimakunduchi katika Kiswahili Sanifu kilichotumika shuleni Makunduchi Zanzibar. Miongoni mwa vipengele alivyochunguza ni maneno ya Kimakunduchi na viambishi vya nafsi. Katika kazi yake aligundua kwamba vitenzi vya lahaja ya Kimakunduchi vina sifa ya kuchukua nafsi katika hali ya umoja na wingi, katika hali ya utenda na utendwa.

Mfano katika lahaja ya Makunduchi nafsi yake ya tatu umoja huwakilishwa na -{ku}-,-{na}- na -{ka}- kwa upande wa utenda, na kwaupande wa utendwa nafsi ya tatu umoja ya lahaja ya Kimakunduchi huwakilishwa na kiambishi -{mu}-.\

Pia Mohamed (kesh) alibainisha njeo zilizokuemo katika lahaja ya Kimakunduchi, na alibaini kuwa kiambishi cha njeo ya Kimakunduchi huwakilishwa na kiambishi -{cha}-, vivyo hivyo hata katika ukanushi pia huwakilishwa na kiambishi -{cha}-. Hivyo inaonekana kwamba utafiti huu ulikuwa ni mwanga katika kazi yetu kwa kuelewa sifa za mofu nafsi katika hali ya umoja na wingi, na utenda na utendwa.

## 2.4 Uelewa wa Wanafunzi katika Vipengele ya Kiisimu

Kuna baadhi ya watafiti walishughulikia upimaji wa uwelewa wa wanafunzi katika vipengele tofauti vya kiisimu, miongoni mwao ni hawa wafuatao:

Ndossi (2001) ambae ameshughulikia matatizo ya uadishi kwa wanafunzi wa Tanzania, Katika utafiti wake aliona matatizo ya uandishi katika lugha ya Kiswahili kwa wanafunzi wa Tanzania, kama vile matumizi ya alamaandishi ambazo ni mkato, nukta mkato, nukta pacha, deshi na matumizi ya herufi kubwa. Mtafiti huyu alibaini kuwa matatizo haya yanatokana na uwelewa mdogo wa watumiaji wa lugha kuwa ni wakati na mahali gani alama zitumike.

Utafiti mwengine ni ule wa Mathooko (2002) ambaye alichunguza matatizo yaliyoikabili lugha ya Kiswahili kama lugha ya kujifunzia isimu katika vyuo vikuu, nchini Kenya,na alibaini kwamba asilimia kubwa ya wanafunzi wa lugha ya Kiswahili vyuoni hawafanyi vizuri katika somo la isimu ikilinganishwa na masomo mengine yanayofundishwa. Kwa hiyo ipo haja ya wanafunzi kuhamasishwa kupenda kujifunza Kiswahili hasa katika nyanja za isimu.

Mohammed (2010) yeye alitafiti matatizo wanayoyapata wanafunzi wa Libya katika kujifunza viambishi vya njeo katika lugha ya Kiswahili. Utafiti wake ulionesha moja wapo ya matatizo yanayowakabili wanafunzi wa Libya wanaojifunza Kiswahili kwa kiasi fulani, pamoja na walimu wanaofundisha lugha hiyo, ili kuweza kuwasaidia hasa wanafunzi kumudu vizuri maswali ya kisarufi ya Kiswahili Sanifu wakati wanapojifunza.

Pia, Uwezo (2010) walifanya utafiti wa kupimauwezo wa watoto mashuleni katika kujifunza kusoma na kuhesabu, kwa watoto wenye umri kati ya miaka (5) na (16). Upimaji ulizangatia mbinu bora iliyoandaliwa na kituo cha ASER nchini India. Matokeo ya utafiti wao yameonesha kwamba muhitimu (1) kati ya (5) hawezi kusoma Kiswahili ngazi ya darasa la pili, pia nusu ya wanafunzi hawawezi kusoma Kiengereza ngazi ya darasa la pili, vilevile mtafiti aligundua kuwa wahitimu (7) tu kati ya (10) wanaweza kufanya hesabu za darasa la pili. Mtafiti aliendelea kubaini kuwa kaya zaidi ya 20000 na watoto zaidi ya 40000 zinaonekana kuwa na matatizo ya elimu Tanzania.

Halkadhalika Obara (2014) alichanganua makosa yanayofanywa na wanafunzi wazungumzaji wa lugha ya Ekegusii na akagundua kuwa miongoni mwa makosa hayo yanatokana na baadhi ya walimu wa Ekegusii ambao wanautendaji mbaya katika uzungumzaji na huchangiakuathiri kwa wanafunzi hao.

Ali (2015) naealichunguza mahusiano baina ya ufundishaji wa stadi ya mazungumzo kwa wanafunzi wa shule za elimu ya awali kisiwani Pemba na kukwama kupata maarifa ya stadi hiyo. Mtafiti alibaini kuwa walimu hawana ujuzi wa kutosha wa

kutumia njia za ufundishaji wa stadi ya mazungumzo na wanafunzi hawajifunzi lugha yao ipasavyo kupitia mazungumzo kutokana na walimu kukosa umahiri katika ufundishaji.

Kimani (2015) aliangalia uwelewa wa wanafunzi kuhusiana na mbinu za ufundishia sarufi na umilisi wa mazungumzo yao, Utafiti huu ulionesha kuwa walimu wengi walitumia mbinu za mhadhara katika kufundishia sarufi ambazo mbinu za kuwashirikisha wanafunzi zilipuuzwa. Pia wanafunzi hawakushirikishwa katika mazoezi yanayoimarisha umilisi wa sarufi na mazungumzo.

Kitsao (2015) aliwachunguza wanafunzi wa shule za msingi kuhusu makosa ya kisarufi katika insha na jinsi yanavyopelekea matokeo mabaya ya mitihani kata ya Ganze, Kaundi ya kilifi, Kenya. Mtafiti alibaini kuwa baadhi ya wanafunzi hawezi kuunda insha kwa kutumia akili zao, kwani hurudia mifano iliyotolewa na walimu wao wakati wakifundishwa.

Nyagah (2016) yeye alichunguza makosa katika kazi andishi za wanafunzi wa shule za upili, Tigama jimbo la Meru, na kukubaini makosa yanayojitokeza kwenye insha za wanafunzikuwa ni ya unazalishaji wa fonimu, udondoshaji wa sauti,uchopekaji wa irabu, na utumiaji wa sauti mbadala, pia aligundua makosa ya uambishaji na unyambuaji pamoja na mlandano wa kiumbo.

Kutokana na maandiko aliyosoma mtafiti hapo juu, inadhihirika kwamba, matokeo ya tafiti hizo yalitoa muongozo mzuri wa kumsaidia mtafiti kuelewa mofu njeo na nafsi katika vitenzi mbali mbali, pamoja na kubaini matatizo mbalimbali

yanayojitokeza kwa wanafunzi katika kujifunza nyanja tofauti za kiisimu.hivyo inaonekana wazi kuwa kazi yetu inauwiano mkubwa na tafiti hizo, kwa vile mtafiti alipima uelewa wa wanafunzi wa matumizi ya mofu nafsi na njeo za Kiswahili kwa wanafunzi wa Zanzibar.Hivyo utafiti mwengine bado unahitajika kutafitiwa ili kuziba mwanya ulioachwa na watafiti waliotangulia, na mwanya huo utazibwa kwa kupima kiwango cha uelewa wa maumbo ya mofu nafsi na njeo za Kiswahili kwa wanafunzi wa Zanzibar, pamoja na kubainisha changamoto za ujifunzaji na ufundishaji wa mofu nafsi na njeo za Kiswahili Sanifu katika shule za Zanzibar.

## 2.5 Pengo la Maarifa

Mtafiti baada ya kusoma kazi zilizotangulia alibaini kwamba kupima uwelewa wa wanafunzi ni jambo muhimu sana katika nyanja mbalimbali za kitaaluma. Kuna tafiti mbalimbali zilizotangulia zinazopima uwelewa wa wanafunzi katika vipengele mbalimbali vya kiisimukama vile Mathooko (2002), Mohammed (2010), Obara (2014) na Kitsao(2015), Kwa hivyo utafiti mwengine unahitajika kufanyika katikakupima kiwango cha uwelewa wa mofu nafsi na njeo za Kiswahili Sanifu kwa wanafunzi wa Zanzibar.

## 2.6 Kiunzi cha Nadharia

Nadharia ni wazo kuu, muongozo mkuu wa mtu au watu wa pahala fulani, wakati fulani, kwa sababu fulani (Sengo, 2009).Hivyo nadharia ndio itakayomuongoza mtafiti katika kuchambua malengo mahsusi ili kufikia malengo ya utafiti.Nadharia zilizomuongoza mtafiti katika kazi yake ni nadharia ya mofofonolojia na nadharia ya Linganuzi, nadharia hizi ndizo zilizotumika katika utafiti huu.

### 2.6.1 Nadharia ya Mofofonolojia

Nadhari ya kwanza iliyotumika katika utafiti huu ni nadharia ya "Mofofonolojia" iliyoasisiwa na baba wa sarufi zalishiNikolaj Trubetzkoy katika mkutano mkuu wa kwanza wa wanafonolololojia wa Ki-slavu ambao ulifanyika Prague mwaka 1929. Trubetzkoy alilitumia neno hili kwa maana ya tawi la isimu linaloshughulikia matumizi ya mofolojia katika kufafanua tofauti fulani za kifonolojia. Nadharia hii ilitumiwa na wataalamu katika kuchanganua vipengele vya kiisimu, baadhi yao ni Bloom field (1930) akitumia msamiati wa Mofofonimiki ikiwa na maana sawa na nadharia ya mofofonolojia ya Trubetzkoy ambayo ilifanya kazi ya kuchunguza mabadiliko ya sauti kwa mahitajio ya kimofolojia katika isimu ya Kimarekani. Pia Hassan (2016) ambae alilinganisha mofu nafsi na njeo katika Kiswahili Sanifu na lahaja ya Kipemba, nadharia hii ilimsaidiakubaini mabadiliko ya kimofofonolojia yanavyoathiri maumbo ya mofu nafsi na njeo katika Kipemba ambayo ndiyo dhima ya nadharia hii.

Kwa mujibu wa Trubetzkoy, mofofonolojia ina kazi kuu tatu. Mosi, kuchunguza muundo wa mofimu katika lugha, pili, kuchunguza mabadiliko ya sauti yanayotokea mofimu zikiungana na tatu, kuchunguza ubadilishanaji wa sauti ambao una uamilifu wa kimofolojia. Kazi hizi ndizo zilizotumika kama ni msingi ya nadharia hii ambayo imetumika katika kuchambua data za lengo la kwanza la utafiti huu. Kutokana na dhima za nadharia hii mtafiti ameona kuwa ni nadharia bora iliyoongoza utafiti huu kutokana na mfanano wake na lengo mahsusi la utafiti huu. Kazi kuu ya mtafiti katika utafiti huu ilikuwani kuangalia kiwango cha uwelewa wa wanafunzi katika kuchambua maumbo ya mofu nafsi na njeo katika Kiswahili Sanifu.

Nadharia ya mofofolojia ilitumika katika kuchambua data za lengo la kwanza tu la utafiti huu lenye kuhitaji kubainisha maumbo ya mofu nafsi na njeo katika Kiswahili sanifu, na kushindwa kuchambua lengo la pili la utafiti huu, ambalo lilitaka kubainisha changamoto za ufundishaji na ujifunzaji wa mada ya mofu nafsi na njeo za Kiswahili,hali hii ilisababisha mtafiti kuongeza nadharia nyengine ambayo ni Linganuzi,yenye uwezo wa kuchambua lengo la pili la utafiti huu.

### 2.6.2 Nadharia Linganuzi

nadharia hii ilianzishwa na Lado mwaka 1957, ni nadhariainayoangalia matatizo tofauti katika kujifunza na ugumu katika kujifunza. Nadharia hii ilitumiwa na Robert Kaplan wa Chuo Kikuu cha Califonia ya Kusini katika miaka ya 1960. Mtafiti alitumia nadharia linganuzikuangalia matatizo ya lugha yaliyoainishwa na wahadhiri katika taasisi ya elimu ya juu ya Amerika, baada ya wanafunzi wengi kutoka katika nchi za Afrika, Asia na Latini Amerika kupata ugumu katika Kiingereza wakati wa kujifunza lugha hiyo. Kwa wanafunzi hao, Kiingereza kilikuwa ni lugha yao ya pili na hivyo kusababisha ugumu katika kujifunza.

Mtaalamu mwengine alietumia nadharia hii ni Ndossi (2001) ambaye ameshughulikia matatizo ya uadishi kwa wanafunzi wa Tanzania, na ilimsaidia kubaini matatizo yanatokana na uwelewa mdogo wa watumiaji wa lugha kuwa ni wakati na mahali gani alama zitumike.

Kutokana na mtafititi kubaibaini kuwa, kuna ugumu katika kujifunza lugha na kuchambua muundo wa lugha, hivyo mtafiti ilimpasa kutumia nadharia linganuzi ili kumsaidia kuchanganua matatizo yanayojitokeza katika ujifunzaji wa lugha ya

Kiswahili kwa wanafunzi wa hapa Zanzibar. Mawazo makuu ya nadharia hii ambayo yalitumika kama ni misingi katika kuchambua data za utafiti huu ni pamoja na:-

i. Lugha inaugumu na changamoto zake katika kujifunza na hasa ikiwa ni lugha ya pili.
ii. Kuna matatizo katika kuchanganua muundo na maumbo yake

Hiyo ndiyo misingi ya nadharia hii iliyotumika kuchambua data zinazohusiana na lengo la pili la utafiti huu.

### 2.7 Muhtasari wa Sura

Katika sura hii mtafiti alichambua kazi tangulizi mbalimbali zinzzohusiana na kazi yake, kama vile jinsi mofu nafsi na njeo zilivyoangaliwa katika lugha za Kibantu na Kiswahili, halikadhalikakuna tafiti zilizoangalia juu ya uwelewa wa wanafunzi katika nyanja za kiisimu. Pia mtafiti alionesha viunzi vya nadharia alivyotumia na vilivyomuongoza katika wake. Sura ya tatu inaelezea mbinu za utafiti.

# SURA YA TATU

# MBINU ZA UTAFITI

## 3.1 Utangulizi

Mbinu za utafiti ni jumla ya Mbinu zote zilizotumiwa katika kufanya utafiti (Kothari, 2004). Kwa hivyo inaonekana wazi kuwa, mbinu za utafiti ni njia za kupata sampuli ya utafiti, kukusanyia data, kuchambua na hata kupanga kazi katika muundo wa kitasnifu, mbinu hizo zilimsaidia mtafiti kukusanya data zilizosahihi kwa lengo la kukamilisha utafiti wake, nazo zikokatika makundi mawili makubwa, ambazo ni mbinu za kukusanyia data na mbinu za kuchambua data.

Sura hii ilizungumziambinu mbalimbali juu ya uchanganuzi na ukusanyaji wa dataambazo zitoa taarifa zakeili kupima uwelewa wa mofu nafsi na njeo za Kiswahili katika shule za za Serekali Zanzibar. Halikadhalika sura hii pia ilionesha eneo la utafiti, uteuzi wa sampuli, pahala utapofanyika utafiti, namna data zilivyokusanywa, walengwa wa utafiti, vifaa vya utafiti vitakavyotumika katika ukusanyaji wa data, vyanzo vya data, mbinu za uchambuzi wa data pamoja na uwasilishwaji wake, na mwishomuhtasari wa sura. Mtafiti alionesha vipengele hivi katika sura hiiili kuwarahisishia watafiti wanaojifunza kuelewa jinsi utafiti unavyotakiwa kufanyika.

## 3.2 Eneo la Utafiti

Utafiti huu ulifanyika katika shule za za Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, katika mkoa wa Mjini Magharibi, kwenye wilaya ya mjini na wilaya ya Magharibi. Ama katika wilaya ya mjini mtafiti aliteua shule 2 kati ya 20, ambazo ni Vikokotoni na Chumbuni, halikadhalika mtafiti aliteua shule mbili 2 kati ya 47 katika wilaya ya Magharibi, shulehizi zilizochaguliwa ambazo ni Bububu na Mtopepo. Mtafiti

aliamua kuteua shule hizi kwa sababu ya kuwepo walengwa wautafiti huu, kwani shule ya Vikokotoni ni shule ya michepuo ikiwemo somo la Kiswahili ambayohufaulisha kwa kiwango kizuri hususan somo la Kiswahili, ama shule ya Chumbuni nishuleyenye kufaulisha katika kiwango cha wastani, hivyo mtafiti alitaka kuonesha utofauti kati ya shule mbli hizi.Kwa upande wa shule ya Bububu na Mtopepo zina idadi kubwa ya wanafunzi kwenye madarasa, ambapo hali hii ilisababishia mtafiti kutaka kuchunguza ili kuelewa ufahamu wao na changamoto wanazokabiliana nazo katika madaya mofu ikiwa kama kipengele cha kiisimu katika lugha ya Kiswahili.

## 3.3 Kundi Lengwa

Cooper (1990) anaeleza kuwa walengwa wa utafiti ni wanachama wote, mtu mmoja, kikundi au elementi ambazo mtafiti amekusudia kuzihusisha katika utafitiwake.Walengwa wa utafiti huuni walimu wanaosomesha somo la Kiswahili na wanafunziwanaosoma somo la Kiswahili katika shule za Zanzibar.

## 3.4 Sampuli na Usampulishaji

Katika sehemu hii tumewasilisha sampuli na usampulishaji wa watafitiwa kama ifuatavyo:

### 3.4.1 Sampuli

Sampuli ni idadi au sehemu ndogo inayotokana na kundi kubwa la watoa taarifa wanaochaguliwa kuwa wawakilishi wa kundi kubwa (Prewitt, 1980). Mtafiti aliteua sampuli iliyomuezesha kujibu maswali yaliyokusudiwa katika utafiti huu. Mtafiti aliteua sampuli ya walimu na wanafunzi wa Kiswahili katika kiwango cha, Utafiti

huu ulikuwa na sampuli ya walimu 24, kila shule ilitoa sampuli ya walimu sita (6). Sampuli ya wanafunzi ilikuwa na jumla ya wanafunzi khamsini na sita (56) ambao wanasoma kidato cha pili, kila shule walitoa wanafunzi kumi na nne (14). Sampuli yote hii iliteuliwa kwa njia ya sampuli ya makusudio kwa kuwalenga walimu na wanafunzi wa Kiswahili na pia iliteuliwa sampuli nasibu kwa kupata sampuli ya utafiti huu miongoni mwa walengwa wa utafiti huu, sampuli hii ilipatikana baada ya mtafiti kuteuashule mbili (2) kati ya ishirini(20) katika wilaya ya mjini ambazo ni Vikokotoni na Chumbuni, na kwa upande wa wilaya ya Magharibi aliteua shule mbili (2) kati ya arobaini na saba (47),ambazoniBububu na Mtopepeo, hivyo mtafiti alitumia njia hii kwa kuepusha idadi kubwa ya watafitiwa ili kupata data zilizo sahihi. Uzuri wa utafiti ni kwa mtafiti kuchagua watoa taarifa wanaofaa kwa utafiti wake (Kothari, 2009). Sampuli ya walengwa inafafanuliwa katika jedwali Na.3.1 kama inavyoonekana hapa chini.

**Jedwali Na.3.1 Sampuli ya Watafitiwa**

| NA. | Jina la Shule | Idadi ya Wanafunzi | Idadi ya Walimu | Jumla |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Chumbuni | 14 | 6 | 20 |
| 2 | Vikokotoni | 14 | 6 | 20 |
| 3 | Bububu | 14 | 6 | 20 |
| 4 | Mtopepo | 14 | 6 | 20 |
| | **JUMLA** | **56** | **24** | **80** |

### 3.4.2 Usampulishaji

Ni mchakato wa kuchagua kundi dogo kutoka kwenye kundi kubwa la watafitiwa ili kufanya makisio ya kundi lengwa (Sign, 2007). Mtafiti aliteuwa njia mbili za usampulishaji katika utafiti huu, ambazo ni usampulishaji nasibu na usampulishaji makusudio.Mtafiti aliteuwa njia ya usampulishaji nasibu kwasababu ilitoa nafasi kwa kila mtu aliekuwemo katika kundi lengwa atakuwa na nafasi sawa ya kuchaguliwa, hivyo njia hii iliondosha upendeleo katika uteuzi wa sampuli.

Pia, mtafiti aliteuwa njia ya usampulishaji makusudio, kwa minajili ya kuteua baadhi ya shule za Zanzibar ambazo ni Vikokotoni, Chumbuni, Bububu na Mtopepo, ziliteuliwa shule hizi kwa sababu ni mchanganyiko wa shule zenye ufaulu wa wastani na zile zenye kutoa matokeo mazuri zaidi katika somo la Kiswahili, ambako kulimsaidia mtafiti kufanya kazi yake kwa ufanisi zaidi. Utafiti huu ulihoji walengwa wachache ambao ni 80ili zipatikane data za usahihi, ukweli huu unathibitishwa na Kothari (1990) kwa kusema kuwa, kuchagua watoa taarifa wachache ni bora zaidi kwa ajili ya kujibu maswali ya ana kwa ana ili kumrahisishia mtafiti kuandika kwa ufupi na haraka kwa kila kinachozungumzwa.

## 3.5 Mbinu za Ukusanyaji Data

Mbinu za ukusanyajia data ni mbinu ambazo mtafiti anategemeakuzitumia wakati wa kukusanya data za utafiti wake, Kothari (1990) anashadidia kwa kusema kuwa, ukusanyaji wa data ni zoezi la awali katika utafiti ambalo humuezesha mtafiti kupata taarifa alizozikusudia ili kumfikisha kwenye malengo yake ya utafiti. Utafiti huu ulitumia mbinu mbalimbali za kukusanyia data, miongoni mwa mbinu hizo ni zile zilizotokana na data za msingi na upili. Data za upili zilikusanywa kwa kutumia

mbinu za maktabani ilhali data za msingi zilikusanywa kwa kutumia mbinu za hojaji na usaili. Njia hizi zilimsaidia mtafiti kupata taarifa za usahihi na uhakika, kwani kuchagua mbinu ya kukusanyia data si kuchagua mbinu yoyote inayoonekana rahisi kutumika bali ni kuchagua mbinu inayojitosheleza na inayohusiana na kile unachokitafiti (Kitchin na Tale, 2000).

### 3.5.1 Hojaji

Hojaji ni miongoni mwa mbinu ya kukusanyia dataambapo mtafiti huandikamaswali na baadae kuyapeleka kwa watoa taarifa ili wayajibu na kurudishiwa mtafiti yakiwa yameshajibiwa(Kothari,1990). Hivyo maswali ya hojaji huhitaji majibu mafupi mafupi au marefu kutokana na mtindo ambao mtafiti anaoutaka kutokana naaina ya taarifa anazohitaji. Aidha mtafiti hutayarisha maswali ya hojaji kwa lengo la kukusanya data. Mugenda na wenzake (2003) anafafanua hoja hii kwa kusema kwambahojaji huandaliwa ili kukusanya taarifa muhimu kutoka kwa watafitiwa.

Maswali ya hojaji yako ya aina mbili ambayo ni hojaji funge yenye kutoa nafasi kwa watafitiwa kuchagua majibu yaliopendekezwa, aidha aina hii huepusha upendeleo na kuwarahisishia watafitiwa katika kujibu hojaji, na kuchangia mtafiti kupata majibu yaliokusudiwa katika kazi yake. Ama aina ya pili ya hojaji ni ile ya yenye maswali huru(maswali yasio funge) ambayo watafitiwa huwa huru kueleza mawazo yao juu ya wanachokifahamu kuhusu walichoelezwa (Kothari, 2008).

Utafiti huu ulitumia aina zote za maswali ya hojaji (funge na huru) kwa sababu kila aina ya maswali ya hojaji iweze kuziba pengo la aina nyengine ya maswali ili

kupunguza mapungufu ambayo yangetokea ikiwa mtafiti angetumia aina moja ya maswali ya hojaji.

Utafiti huu ulitumia mbinu hii ya hojaji kwa kuvitayarisha vitenzi vya Kiswahili Sanifu ambavyo mtafiti alivipata kutoka katika vitabu vya Kiswahili, makamusi ya Kiswahili Sanifu na hata katika tasnifu mbalimbali. Kazi hii ilitumia hojajikwa sampuli ya wanafunzi. Mtafiti alitumia mbinu hii kwa sampuli ya wanafunzi ili kuwapa fursa ya kufikiria jawabu na hata kupata muda wa kufanya rejea juu ya maswali waliyoulizwa. Mbinu hii ilitumika kwa sampuli ya wanafunzi 56.

Hojaji lilimsaidia mtafiti kupata matokeo ya lengo la kwanza na la pili lenye kutaka kuainishakiwango cha uelewa wamaumbo ya mofu nafsi na njeo za Kiswahili sanifukwa wanafunzi wa Zanzibar pamoja na kubainisha changamoto za ujifunzaji na ufundishajiwa mofu nafsi na njeo za Kiswahili Sanifu kwa shule za Zanzibar.

### 3.5.2 Usaili

Usaili ni njia ya mazungumzo ya ana kwa ana au kwa njia ya simu,na msailiwa huweza kujibu kwa njia ya mdomo, kama anavyoelezea Enon (1998) kuwamahojiano ni mbinu ya kuuliza maswali ya ana kwa ana, simu, au barua pepe, kati ya watu wawili au zaidi, kwa lengo la kukusanya taarifa au maoni kuhusu swali la utafiti lililoainishwa.

Mtafiti aliona ni vyema atumie njia ya ana kwa ana, kwani ilikuwa ni rahisi kwake kuwapata kundi lengwakwa wepesi. Pia, alitumia usaili huru, kwa sababu mtafiti aliandaa maswali maalum kwa ajili ya walengwa, pamoja na maswali mengine ya

ziada ambayo yalihitaji ufafanuzi wa jambo linapohitajika. Katika njia hii mtafiti alitumia walimu ishirini na nne (24) kwa kuchukua sampuli ya walimu sita kwa kila shule teule. Njia hii ilikuwa ni bora kwa walimu kwa sababu tulipata fursa ya kujadili mambo mengi tena kwa wasaa, pia ni njia ambayo haimkwazi mwalimu kwa kuchukua mzigo wa dodoso, swali ambalo hulilalamikia kukosa muda wa kulijaza na hata kulipoteza kutokana na harakati zao.

### 3.5.3 Mbinu ya Maktabani

Mbinu hii inahusisha mapitio ya kazi mbalimbali zilizofanywa na watafiti waliotangulia zenye kuhusiana na kazi hii. Kazi hizo kuhusu nadharia mbalimbali au hata uchambuzi wa dhana zinazohusiana na mada ya utafiti husika kwa namna moja ama nyengine (Kothari, 1990).

Mtafiti alitembelea katika maktaba mbalimbali ili kutalii maandishi tofauti yenye kuhusiana na kazi yake. lengo la mtafiti ni kuagalia mawazo ya wanaisimu wenginewameeleza nini kuhusiana na mada hii ya utafiti. Njia ya maktaba ni ilimsaidia sana mtafiti kujifunza mengi yaliyomo kwenye kazi za wenzake pamoja na kuangalianadharia na mbinu kadhaa zilizohusiana na utafiti huu, na pia mtafiti alipata data za upili kutokana na maandiko hayo.

## 3.6 Mbinu za Uchambuzi wa Data

Uchambuzi wa data ni kitendo cha kufupisha na kupangilia vizuri data zilizokusanywa kwa namna ambayo iliwezesha kukamilisha malengo ya utafiti (Babbie, 1999).

Uchambuzi wa data hufafanuliwa kwakutumia mikabala ya aina mbili ambayo; ni mikabala wa kiidadi na ule wa maelezo. Kwa mujibu wa Enon (kesh) mkabala wa kimaelezo ni mbinu ya kuchambua na kufafanua data ambapo mtafiti hueleza na kubainisha data zake kwa kutumia maelezo.Ama kwa upande wamkabala wa kiidadi ulielezewa na Kothari (2008) kwamba ni ile inayohusisha tarakimu kama vile asilimia, idadi za watafitiwa, majedwali na michoro inayotokana na data za kihesabu.

Utafiti huu ulitumia njia mchanganyiko katika uchambuzi wa data, njia hizi zilimsaidia mtafiti kuweka wazi taaarifa ambazo zilihitaji ufafanuzi kwa kina na zile zilizohitaji idadi. Mbinu hizi za uchambuzi wa data zimekuwa muafaka katika utafiti huu kwasababu imeendana na aina ya utafiti wetu. Mtafiti alitumia njia hizi kwa lengo la kupata kiwango cha ufahamu wa wanafunzi kiasilimia na kuchambua kwa maelezo ili kupata taarifa za usahihi na matokeo mazuri, kama Haji (2015) alivyowanukuu Best na Khana (1993) kwa kusema; mbinu moja haijitoshelezi katika kupata data zinazotumika na kukubalika katika utafiti.

## 3.7 Maadili ya Utafiti

Maadili ni kawaida zinazoelezea tabia zetu katika mahusiano yetu ya kila siku na wenzetu (Mathooko, 2007). Mtafiti ili afanikishe kazi yake vizuri ni lazimakuwaelezea na kuwafafanulia maadili kwa watafitiwa ili watoe taarifakwa uhuru nausahihi. Hali hii ilijenga mashirikiano makubwa tena bila ya woga kwa wale waliaopata nafasi ya kuwa sampuli katika kazi hii. Katika utafiti huu mtafiti alizingatia mambo yafuatayo:

Aliwaeleza watafitiwadhamira ya utafiti huu kuwa ni “upimaji wa uelewa wa matumizi ya mofu nafsi na njeo za kiswahili Sanifu kwa wanafunzi wa Zanzibar”, mtafiti aliwaarifu walengwa dhamira hiyo ili kuweza kujitayarisha vizuri kwa ajili ya kuchangia kwa upana na uwazi kwa kutoa data sahihi kwa ridhaa yao juu yauchambuzi wa mofu nafsi na njeo za Kiswahili.

Pia, mtafiti aliwahakikishia watafitiwa taarifa zao kuwa siri na kutumika kwa shughuli za utafiti huu tu na sivinginevyo.

## 3.8 Muhtasari wa Sura

Katika sura hii ya tatumtafiti alizungumzia vipengele na mbinu mbalimbali za ukusanyaji na uchambuzi wa data, eneo la utafiti, walengwa wa utafiti, sampuli na usampulishaji. Njia alizozitumia mtafiti ambazo zimempatia data stahilini njia ya mahojiano, hojaji na maktabani. Kwa hivyo kumalizika kwa sura hii inafuata sura ya nne inayokuhusu uwasilishaji na uchambuzi wa data za utafiti.

# SURA YA NNE

# UWASILISHAJI NA UCHAMBUZI WA DATA

## 4.1 Utangulizi

Sura hiiimezingatia uwasilishaji na uchambuzi wa data zilizopatikana kutokana na wadadisiwa na wasailiwa wa mahojiano yahusuyo “upimaji wa uelewa wa matumizi ya mofu nafsi na njeo za Kiswahili kwa wanafunzi wa shule za Zanzibar”. Sura hii ilizingatia malengo ya utafiti,lengo kuu na Malengo mahsusi ambayo nikuainisha kiwango cha uelewa wa maumbo ya mofu nafsi na njeo katika Kiswahili Sanifupamoja na kubainisha changamoto za ujifunzaji na ufundishaji wa mofu nafsi na njeo za Kiswahili Sanifu katika shule za Zanzibar. Sura hii ilitumia mikabala miwili ya uchambuzi wa data, mmoja kati ya mikabala hiyo ni ule wa kitakwimu ambao data zilipatikana kwa kutumia mfumo wa komputa (SPSS) pamoja na “excel”, mkabala wa pili ni ule wa maelezo ambao mtafiti ulimpatia data kwa ufafanuzi wa maelezo na kupima matokeo kwa kutumia kiunzi cha nadharia ili kufikia hitimisho.

Data hizo zilikusanywa mashuleni kwa kuwahusisha walimu na wanafunzi wa shule nne za za Mkoa wa Mjini Magharibi Unguja. Jumla ya watafitiwa wote walikuwa ni80, mahojiano yamefanywa kwa kutumia njia ya dodoso na mahojiano ya anakwaana (mubashara), kwa kuhusisha wanafunzi56 na walimu 24, ambao ni sawasawa na asilimia 100 kwa watafitiwa wote.

Katika utafiti huu mtafiti amechambua data kwa kutumia njia mbili ambazo ni njia ya kitakwimu na njia ya maelezo kwa kufafanua na kutoa matokeo ili kufikia hitimisho kutokana na viunzi vya nadharia. Uchambuzi kwa kutumia njia ya

kitakwimu unaonesha idadi ya wahojiwa na wadadisiwa kwaasilimia zao na ule wa maelezo umetumika kwa kufafanua na kutoa matokeo ili kufikia hitimisho kutokana na viunzi vya nadhariaalivyotumia mtafiti ambavyo ni mofofonolojia na linganuzi.

## 4.2 Kiwango cha Uelewa wa Maumbo ya Mofu Nafsi na Njeo Katika Kiswahili Sanifu

Lengo la kwanza la utafiti huu lilikuwa “kuainisha kiwango cha uelewa wa maumbo ya mofu nafsi na njeo katika Kiswahili Sanifu kwa wanafunzi wa Zanzibar. Katika kufikia lengo hili mtafiti alitumia njia ya usaili kwa walimu ishirini na nne (24) na hojaji kwa wanafunzi khamsini na sita (56). Njia hizi zilitumika katika ukusanyaji wa data za utafiti huu kama ilivyochambuliwa hapo chini kwa kila njia.

### 4.2.1 Uwasilishaji wa Data

Utafiti huu umetumia njia tatu katika ukusanyaji wa data ambazo ni; njia ya usaili, njia ambayo imetumika kwa sampuli ya walimu na njia ya hojaji njia iliyotumika kwa sampuli ya wanafunzi, pia mtafiti alitumia njia maktabani ili kupata data za upili. Njia hizi zimefafanuliwa tofauti kama zilivyochambuliwa hapo chini.

#### 4.2.1.1 Njia ya Hojaji

Wanafunzi 56 sawa na 70% walishiriki kwenye utafiti huu kwa kutoa taarifa zinazostahili katika kazi yetu, kama inavyojionesha kwenye jedwali Na.4.1 hapo chini.

**Jedwali Na. 4.1 Viwango vya Elimu, Jinsia na Shule Walizotokea Wahojiwa**

| **Shule** | **Jinsia** | **Mwanafunzi** | **Walimu** | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | **Kidato cha Pili** | **Shahada ya Uzamili** | **Shahada** | **Stashahada** | **Jumla** |
| Bububu | Mke | 8 | 1 | 1 | 1 | 3 |
| | Mme | 6 | 0 | 2 | 1 | 3 |
| Chumbuni Sekondri | Mke | 6 | 0 | 2 | 1 | 3 |
| | Mme | 8 | 0 | 2 | 1 | 3 |
| Mtopepo | Mke | 7 | 1 | 1 | 1 | 3 |
| | Mme | 7 | 0 | 2 | 1 | 3 |
| Vikokotoni Sekondaari | Mke | 7 | 1 | 2 | 1 | 4 |
| | Mme | 7 | 0 | 2 | 0 | 2 |
| JUMLA | | 56 | 3 | 14 | 7 | 24 |
| **Asilimia** | | **70** | **Asilimia** | | | **30** |

Watafitiwa hawa walikuwa 80 kama sampuli ya utafiti huu inavyoeleza. Hivyo sampuli ya walimu na wanafunzi iliweza kushiriki katika utafiti huu kwa asilimia mia moja (100%).

#### 4.2.1.2 Njia ya Usaili

Utafiti huu ulitumia njia yausaili katika kufikia sampuli ya walimu. Jumla ya walimu ishirini na nne (24) sawa na 30% walishiriki moja kwa moja katika utafiti huu kwa kusailiwa na mtafiti. Ushiriki wa walimu ulikuwa katika viwango tofauti uliomuezesha mtafiti kuona kile ambacho ameamua kukifanyia utafiti kama inavyojionesha kwenye jedwali Na.4.1.

Kwahivyo inadhihirika wazi kwamba walimu wotewaliohojiwa ambao ni sawa na 100% ni walimu wanaofundisha somo la Kiswahili katika shule za .

#### 4.2.1.2.1 Walimu Waliosomea Fani la Kiswahili na Kukifundisha

Mtafiti alihitaji kuelewa walimu waliosomea fani ya Kiswahili kwa lengo la muendelezo wa kazi yake, kama swali la 1 katika mahojiano ya walimu lilivyohitaji, hivyo. Jedwali Na.4.2 inaonesha idadi ya walimu waliosomea fani ya Kiswahili na pia wanasomesha Kiswahili.

**Jedwali Na.4.2 Walimu Waliosomea Fani ya Kiswahili na Kukifundisha**

| **Walimu** | **Idadi** | **%** |
|---|---|---|
| Waliosomea | 22 | 92 |
| Wasiosomea | 2 | 8 |
| **Jumla** | **24** | **100.0** |


Katika swali hili kwenye mahojiano ya walimu kwenye swali la 1, mtafiti alibaini kwamba walimu wa Kiswahili waliohojiwa ambao wanafundisha somo la Kiswahili na wamesomea fani ya Kiswahili ni watafitiwa 22 ambao sawa na 92%, na watafitiwa 2 sawa 8% hawa wanasomesha Kiswahili lakini si walimu wa fani ya Kiswahili kwani hawakusomea fani ya Kiswahili lakini wanao uwezo wa kusomesha somo la Kiswahili, pamoja na kwamba hawakusomea fani ya Kiswahili walikuwa wakipata mafunzo maalum ya mara kwa mara juu ya somo la Kiswahili yanayohusiana na mada wanazozifundisha.

Kwahivyo utafiti umeonesha wazi kuwa walimu wanauzoefu wa kutosha wa miaka mingi, sambamba na viwango vizuri vya elimu walivyonavyo, jedwali Na. 4.1 hapo juu linaonyesha viwango vya elimu vya walimu waliohojiwa.

**4.2.1.2.2 Uzoefu wa Kufundisha Somo la Kiswahili**

Walimu wote walioshriki katika utafiti huu ni wale ambao wanafundisha somo hili kama ilivyoonekana kwenyejedwali Na. 4.2 hapo juu.

Katika kipengele hiki kilichoshughulikia muda wa uzoefu wa kufundisha somo la Kiswahili, matokeo yake ni kama yanavyojidhihirisha kwenye chati Na. 4.1




**ChatiNa.4.1Uzoefu wa ufundisha somo la Kiswahili**

Chati Na. 4.1 linaonyesha muda wa uzoefu wa ufundishaji mada ya mofu katika lugha ya Kiswahili, kimtazamo walimu wanauwezo mzuri wa kufundisha kwa vipimo vya viwango vyao vya kielimu na uzoefu wa ufundishaji, hivyo Utafiti uligundua kuwa walimu7 (29.2%) wana muda wa uzoefu wa miaka 1 – 3 wa

ufundishaji somo la Kiswahili, pia walimu 5 (20.8%) wanamuda wa miaka 4 – 6 ya ufundishaji. Vile vile, idadi ya walimu 5 (20.8%) wanamuda mrefu wa kufundisha miaka 10 na zaidi, halkadhalika walimu 4 (16.7%) pia wanaoneka kuwa na muda mrefu wa kufundisha somo la Kiswahili kwa miaka 7 – 9, aidha watafitiwa 3 (12.5%) wanauzoefu wa muda mfupi chini ya mwaka mmoja wa kufundisha somo la Kiswahili.Kutokana na takwimu hizo kama inavyoonekana kwenye chati, mtafiti aligundua kuwa muda wa kufundisha chini ya mwaka 1 wanaonekana kuwa walimu wachache (12.5%) ndio wanaofundisha somo la Kiswahili, lakini pia muda wa mwaka 1 hadi 3 ndiyo kiwango kikubwa cha walimu cha (29.2%) wanaofundisha somo la Kiswahili kwenye shule za Zanzibar, na huu ni muda wa kutosha kwa kupata taarifa na ubobezi wa kutatua changamoto zinazohusiana na mada ya mofu.

### 4.2.2 Kiwango cha Uwelewa waUchambuzi wa Maumbo ya Mofu

Katika kipengele hiki mtafiti alihitaji kuelewa uwezo wa wanafunzi wa kuchambua maumbo ya mofu kwa kuzingatia mofu njeo na mofu nafsi wakati wa somo linapofundishwa.

#### 4.2.2.1 Kiwango cha Uwelewa Katika Uchambuzi Mofu Nafsi na Njeo

Utafiti ulibaini kuwa wanafunzi wengi wamekuwa na mwamko juu ya mada ya mofu iliyohusisha mofu nafsi na njeo. Pia utafiti uligunguai mitazamo tofauti ya uchambuzi wa maumbo ya mofu ambao umepatikana na data zake kuchambuliwa kwa misingi ya nadharia ya mofofonoloji; miongoni mwa misingi iliyotumika, kwanza ni suala la kuchunguza muundo wa mofimu katika lugha. Pili, kuchunguza mabadiliko ya sauti yanayopatikana mofimu zikiungana na tatu, kuchunguza ubadilishaji wa sauti ambao una uamilifu wa kimofolojia. Mitazamo hii imepatikana

baada ya majibu ya swali la 6 lililoulizwa kwa watafitiwa katika mahojiano kuhusiana na uwezo wa uchambuzi wa matumizi ya mofu nafsi na njeo wakati wa ufundishaji huwa katika kiwango gani? Majibu yalikuwa kama inavyojionesha kwenye jedwali Na. 4.3.

**Jedwali Na.4.3 Uwezo wa Wanafunzi wa Kuchambua Maumbo ya Mofu Nafsi na Njeo Wakati wa Kufundisha**

| **Kiwango cha uwezo** | **Idadi ya Waliofanya** | **%** |
|---|---|---|
| Mkubwa sana | 5 | 20.83 |
| Wastani | 9 | 37.5 |
| Mdogo | 6 | 25 |
| Mdogo Sana | 4 | 16.67 |
| **Jumla** | **24** | **100** |

Katika swali hili mtafiti aliwahoji walimu katika shule za alizoziteua, kama inavyoonekana katika jedwali Na. 4.4 hapo juu.

Katika swali la kupima uwezo wa wanafunzi wa kuchambua matumuzi ya mofu ya nafsi na njeo, utafiti ulibaini kuwa kiwango chaocha uchambuzi ni wastani. Matokeo haya yanatokana na takwimu zilizokusanywa katika utafiti huu, ambazo zimechambuliwa katika jedwali la hapo juu linalofafanua kwamba watafitiwa 3 kati ya watafitiwa 24 katika sampuli ya walimu waliojibu swali hili ambao ni sawa na 18.75% walieleza kuwa uwezo wa wanafunzi kuchambua matumizi ya mofu nafsi na njeo ni mkubwa sana, watafitiwa 7 sawa na 43.75% waliona kuwa uwezo wa

wanafunzi wa kuchambua matumizi ya mofu ni yawastani, pia watafitiwa 4 sawa na 25% wameona kuwa uwezo wa wanafunzi kuchambua matumizi mofu ni mdogo. Hata hivyo watafitiwa 2 sawa na 12.5% wameeleza kuwa kiwango cha uchambuzi wa matumizi ya mofu kuwa ni mdogo. Maelezo haya yalitokana na baadhi ya wanafunzi kushindwa kuchambua muundo wa mofimu katika lugha wakati mwalimu anapofundisha. Aidha maelezo haya yanatokana na msingi wa nadharia ya mofofonolojia ya kuwa umahiri wa mtu katika mofolojia unatokana na uwezo wa kuchunguza muundo wa mofimu katika lugha.

#### 4.2.2.2 Idadi ya Viambishi Vinavyowakilisha Mofu njeo Katika Kiswahili Sanifu

Inafahamika kwamba katika lugha ya Kiswahili Sanifu kunanyakati tatu za mofu njeo, suala la msingi lilihitajiidadi ya nyakati za mofu njeo, swali hili liliulizwa kama hivi ifuatavyo *“kuna viambishi vingapi vinavyowakilisha mofu njeo katika Kiswahili sanifu?”* katika suala hili wanafunzi walikuwa na majibu tofauti kama yafuatavyo kwenye jedwali Na.4.4 Uwelewa wa Viambishi Vinavyowakilisha Mofu Njeo.

**Jedwali Na. 4.4 Uwelewa wa Viambishi VinavyowakilishaMofu Njeo**

| Idadi viambishi njeo | Kiasicha Uelewa | % |
|---|---|---|
| Vitatu | 32 | 57.14 |
| Vine | 15 | 26.79 |
| Vitano | 9 | 16.07 |
| **Jumla** | **56** | **100.00** |

Mifano iliyojiri kwenye masuali hayo

- Wakati uliopita mfano, a**li**kwenda
- Wakati uliopo mfano, a**na**kwenda
- Wakati ujao mfano, a**ta**kwenda

Maelezo haya yanadhihirisha kuwa wanafunzi thelathini na mbili (32) kati ya wanafunzi khamsini na sita (56)wanaweza kuchunguza mabadiliko ya sauti katika vitenzi, mabadiliko ambayo yanatokana na mofimu ya njeo na kuunda mofu kutokana na nyakati tofauti, asilimia kubwa ya wahojiwa na wale walioshiriki kwenye utafitiwalionesha kuelewa nyakati kwa kueleza kwamba kuna viambishi vitatu vyanjeo katika lugha ya Kiswahili ambazo ni wakati uliopita, wakati unaoendelea na wakati ujao. Habwe na Karanja (2004) na Kihore (2003) ni wanaisimu waliozungumzia juu ya viambishi vinavyowakilisha mofu njeo katika Kiswahili kwamba ziko tatu ambazo huwasilishwa na mofu tofauti. Hata Matinde (2012) piaalieleza kwamba viambishi vinavyowakilisha mofu njeo vipo vya wakati uliopo (na), wakati ujao (ta), na wakati uliopita (li) / (me). Rubanza (2003) anatafautiana na wenziwe kutokana na yeye kubainisha kuwa mofu njeo ziko 15 kwa wakati tofauti na baadhi hazitumiki katika Kiswahili sanifu, na hutumika katika lahaja za Kiswahili.

#### 4.2.2.3 Idadi ya Viambishi Vinavyowakilisha Mofu Nafsi katika Kiswahili Sanifu

Hali za mofu nafsi katika lugha ya Kiswahili inasemwa kuwa ziko tatu na wengine wanasema kuwa ziko sita kikubwa kilichojitokeza hapa nikwamba kila aina moja ya hali imejigawa kwenye sehemu mbili yaani umoja na wingi.

Asilimia kubwa ya watafitiwa walionesha kuelewa kwamba kuna viambishi vitatuvya nafsi katika lugha ya Kiswahili sanifu, ambazo ni nafsi ya kwanza, nafsi ya pili na nafsi ya tatu. Data zilizokusanywa zinavyooneshwa kwenye jedwali Na. 4.5 hapo chini.

**Jedwali Na.4.5 Uwelewa wa Viambishi VinavyowakilishaMofu Nafsi**

| **Idadi ya viambishi nafsi** | **kiasi cha uelewa** | **%** |
|---|---|---|
| Vitatu | 34 | 60.71 |
| Vine | 9 | 16.07 |
| Sita | 13 | 23.21 |
| **Jumla** | **56** | **100.00** |

Jedwali Na. 4.6 linaonyesha kuwa watafitiwa34 ambao ni 60.71% katka sampuli ya walimu wanaongoza kwa kukubaliana kuwa viambishi vya nafsi vipovitatu. Kundi fuatishi ni lile la uelewa wa kuwa viambishi nafsi ni sita kwa idadi ya watafitiwa 13 sawa na 23.2%, kundi hili lilielewa idadi ya 6 kwasababu ya kuvunja njeo kwenye idadi ya umoja na wingi, na kundi la mwisho ni la idadi ya watafitiwa 9 sawa na 16.07 % kuwa na uwelewa wa viambishi nafsi kuwa ni vine.

Mifano ya mofu nafsi katika lugha ya Kiswahili Sanifu ambayo ilitolewa kwenye majibu

- *Nafsi ya kwanza mfano, ninaimba (umoja), tunaimba (wingi)*
- *Nafsi ya pili mfano, unaimba (umoja), munaimba (wingi)*
- *Nafsi ya tatu mfano, anaimba (umoja), wanaimba (wingi)*

Mifano hii inadhihirisha kuwa wanafunzi wengi wanaweza kuchunguza mabadiliko ya sauti katika maneno ya lugha ya Kiswahili, mabadiliko ambayo yanatokana na mofimu ya nafsi na kuunda mofu kutokana na nafsi ya mtendaji. Hali hii inadhihirisha kiwango chao cha umahiri kutokana na msingi wa nadharia ya mofofonolojia unaoeleza kuwa umahiri wa wanafunzi unatokana na uwezo wa kuchunguza mabadiliko ya sauti yanatokana na muunganiko wa mofimu.

Kwahivyo viambishi vya nafsi viko vitatu ambavyo ni nafsi ya kwanza ya pili na ya tatu, dai hili linadhihirika paleRubanza (2003) alivyoelezakwamba kuna nafsi tatu katika Kiswahili, nafsi ya kwanza,nafsi ya pili na nafsi ya tatu, na hutegemea umoja na wingi.  Kwa mfano:

| **Nafsi** | **Mofu Nafsi** | **Kitenzi** |
|---|---|---|
| N1 | -ni-  U | -ni-  ninasoma |
| | -tu-  W | -tu- tunasoma |
| N2 | -u-   U | -u- unasoma |
| | -m-  W | -w- mnasoma |
| N3 | -a-   U | -a-  anasoma |
| | -wa-W | -wa- wanasoma |

#### 4.2.2.4 Dhana ya Mofu na Mofimu

Watafitiwa waliulizwa juu ya maana ya mofimu na mofu katika taaluma ya isimu ya lugha ya Kiswahili. Watafitiwa wote  walijibu swali hili, na kwa jumla walitoa maana ya istilahi hizi ambazo zinafanana kutokana na dhana zote hizi kujumuisha dhana na istilahi za msingi katika maana hizo. Kwa upande wa mofimu wanaeleza kuwa mofimu ni kipashio kidogo cha kisarufi chenye kuleta maana. Ama kwa upande wa mofu, watafitiwa walijibu kuwa mofu ni kipashio kidogo cha kisarufi kinachostiri mofimu.

Kwa jumla, utafiti ulijumuisha maana za dhana hizi kwa kueleza kuwa mofu ni kipashio kidogo cha kisarufi ambacho hakileti maana. Tafsiri au maana hii inaenda sambamba na Massamba (2004) kwa kueleza kwamba mofu ni umbo kamili ambalo huwakilisha mofimu na hudhihirika kifonolojia na kiothografia. Hivyo dhana hii inaonekana kuwa na mfanano mkubwa na dhana ya mtafiti. Kwa mnasaba huu walimu wa somo la Kiswahili inatupasa kuelewa kwa undani dhana ya mofu na mofimu, kwa lengo la kuwaongoza wanafunzi kuzielewa kwa uwazi dhana hizi.

#### 4.2.2.5 Uchambuzi wa Maumbo ya Mofu Nafsi kwenye Vitenzi

Katika swali la 3a kwenye hojajiza wanafunzi ambao walichambua maumbo ya mofu nafsi ili kufikia lengo la kwanza la utafiti huu ambalo linahitaji kuainisha kiwango cha uwelewa wa maumbo ya mofu nafsi za Kiswahili sanifu.

Utafiti ulibaini kuwa uchambuzi mofu na mofimu kwa jumla katika lugha hutegemea sana muundo wa sentensi na meneno yaliyomo kwenye sentensi hiyo. Uchambuzi huu unachambuliwa kupitia vitenzi mbambali katika hojaji za watafitiwa 56. Kama inavyonekana kwenye jedwali Na. 4.6 hapo chini.

**Jedwali Na. 4.6 Uchambuzi wa Mofu Nafsi Kwenye Vitenzi**

| Vitenzi | Mofu Nafsi | | | % ya jibu shihi | % ya waliojaribu na Waliokosea |
|---|---|---|---|---|---|
| | Jibu sahihi | Waliojaribu | Waliokosea | | |
| Ninakwenda | "Ni" nafsi ya kwanza umoja (45) | "Ni" nafsi (5) | Kakosea (6) | 80.36 | 19.64 (8.93+10.71) |
| Mtaimba | "Mu" nafsi ya pili wingi (47) | "Mu" nafsi (7) | Kakosea (2) | 83.92 | 16.07 (12.5+3.57) |
| Unaimba | "U" nafsi ya pili umoja (19) | "na" nafsi (23) | Kakosea (14) | 33.92 | 66.07 (41.07+25) |
| Tunakwenda | "Tu" nafsi ya kwanza wingi (27) | "na" nafsi (14) | Kakosea (15) | 48.21 | 51.79 (25+26.79) |
| Watalia | "Wa" nafsi ya tatu wingi (25) | "Wa" nafsi (14) | Kakosea (17) | 44.64 | 55.36 (25+30.36) |
| Alilia | "A" nafsi ya tatu umoja (26) | "A" nafsi (17) | Kakosea (13) | 46.42 | 53.57 (30.36+23.21 |

Kutokana na jedwali la hapo juu, matokeo yanaonekana kupitia sampuli ya wanafunzi, katika kitendo **Ninakwenda,** waliojibu sahihi niwatafitiwa 45 sawa na80.36%, waliojaribu ni watafitiwa 5 sawa na 8.93%, pia wapo waliokosea kabisa ambao ni watafitiwa 6 sawa na10.71%. Hii inaonekana kwamba katika kitendo“***Ninakwenda”*** katikanafsi ya kwanza umoja**,** licha ya wanafunzi wengikujibu sahihi lakini pia wapo wanafunzi wachache ambao wamekoseakabisa.Kwa upande wa kitendo cha **Mutaimba,** watafitiwa 47 sawa na 83.92% wamejibu sahihi, hata hivyo watafitiwawaliojaribu takriban ni 7 sawasawa na 12.5% na waliokosea ni watafitiwa 2 ambao sawa na 3.57%. Ni dhahiri kwamba katika kitendo **Mutaimba,** wanafunzi wengi walijaribu kuchambua mofu nafsi ya

pili umoja”, ingawa baadhi ya wanafunzi walijaribu kuchambua lakini hawakukamilisha uchambuzi huo.

Tukiangalia kitendo **Unaimba,** matokeo yanaonesha kwamba watafitiwa 19 ambao sawa na 33.92% walijibu kwa usahihi, pia watafitiwa 23 sawa na 41.07% walijaribuna watafitiwa 14 sawa na 25% walikosea kuchambua mofu nafsi katika kitendo hicho. Tafsiri ya matokeo haya inaonekana kwamba, nafsi ya pili umoja watafitiwa wachachewalijibu kwa usahihi, hali hii inamaanisha kuwa wanafunzi wengi hawaelewi uchambuzi wa nafsi ya pili umoja, licha ya kuwa wapo wanafunzi waliojaribu.

Kitendo **Tunakwenda** kwa nafsi ya kwanza wingi, matokeo yake yanaonesha kwamba watafitiwa 27 sawa na 48.21% wamejibu kwa usahihi, watafitiwa14 wamejaribu ambao ni sawa na 25%, na watafitiwa 15 sawa 26.795% wamekosea kabisa kuchambua nafsi ya kwanza wingi. Mtafiti alibaini kwamba wanafunzi waliowengi wameelewa vyema uchambuzi wa nafsi ya kwanza wingi, ingawa wapo ambaowamekosea kama inavyoonekana katika jedwali 4.9 hapo juu. Halikadhalika kitendo **Watalia** kwa nafsi ya pili wingi, inaonekana kwamba watafitiwa 25 sawa na 44.64% walijibu kwa usahihi, watafitiwa 14 sawa na 25% walijaribu na wanafunzi 17 ambao sawa na 30.36% walikosea, hivyomtafiti alibaini kuwa baadhi ya wanafunzi bado hawana uwelewa mzuri wa nafsi ya pili wingi, kama tunavyoona katika jadweli hapo juu.Katika kitendo **Alilia** kwa nafsi ya tatu umoja, watafitiwa 26 sawa na 46.42% walijibu kwa usahihi, watafitiwa17 sawa30.36% walijaribu na watafitiwa 13 sawa na 23.21% walikosea kuchambua mofu nafsi katika kitendo cha **Alilia.** Kutokana na takwimu za kipengele hiki, mtafiti alibaini kuwa wanafunzi

wengi wanaelewa nafsi ya tatu umoja, licha ya kuwa kuna baadhi ya wanafunzi waliokosea ambao inadhihirika kuwa hawaelewi kabisa nafsi ya tatu umoja.

Mfano sahihi wa mofu nafsi katika kitendo “**Alilia”**

| | | |
|---|---|---|
| “A” | inaonesha nafsi ya tatuumoja. | Jibu sahihi |
| “A” | inaonesha nafsi. | Amejaribu |
| “A” | inaonesha nafsi yapili umoja. | Amekosea |

Taarifa za hapo juu katika jedwali Na. 4.9 zinadhihirisha uchambuzi wa mofu nafsi katika vitenzi vya Kiswahiliupo katika kiwango cha wastani nzuri wa 56.25%. Hoja hii inatokana na uchambuzi wa takwimu za hapo juu pamoja na kuthibitishwa na misingi ya nadharia ya mofofonolojia inayozingatia kuwa umahiri wa wanafunzi katika mofolojia unatoakana na uwezo mzuri wa kuchambua muundo wa mofimu katika lugha pamoja na kuchunguza mabadiliko ya sauti yanayojitokeza katika maneno ili kuunda mofu katika neno hilo kutokana na mofimu ya aina moja. Hivyo kutokana na uwezo wa wanafunzi wa kuchambua mofu nafsi kutokuwa wa kina na wenye kujitosheleza, utafiti ulitathimini na kujumuisha kuwa wanafunzi ni wenye kiwango cha wastani katika uchambuzi wa mofu nafsi.

#### 4.2.2.6 Uchambuzi wa Mofu Njeo Kwanye Vitenzi

Katika kipengele hiki mtafiti aliweza kuchambua data tofauti zinazotokana na sampuli ya wanafunzi waliochambua maumbo ya mofu njeo kama swali 3b kwenyehojaji ya wanafunzi lilivyohitaji kuainisha maumbo ya mofu njeo, jedwali Na.4.7 linafafanua zaidi hapo chini.

**Jedwali Na. 4.7 Uchambuzi wa Mofu Njeo Kwenye Vitenzi**

| Vitenzi | Njeo | | | % ya jibu sahihi | % ya waliojaribu na waliokosea |
|---|---|---|---|---|---|
| | Jibu sahihi | Waliojaribu | Waliokosea | | |
| Ninakwenda | "na" Njeo ya wakati unao endelea (43) | "na" njeo ya wakati(4) | Kakosea(9) | 76.78 | 23.21 (7.14+16.07) |
| Mtaimba | "ta" Njeo ya wakati unaokuja(4) | "ta "njeo ya wakati(29) | Kakosea (23) | 7.14 | 92.86 (51.79+41.07) |
| Unaimba | "na" Njeo ya wakati unaoendelea (31) | "na" njeo ya wakati (14) | kakosea(11) | 55.35 | 44.64 (25+19.64) |
| Tunakwenda | "na" Njeo ya wakati unaoendelea (34) | "na" njeo ya wakati(6) | kakosea(16) | 60.71 | 39.28 (10.71+28.57) |
| Watalia | "ta" Njeo ya wakati ujao (34) | "ta "njeo ya wakati(9) | kakosea(13) | 60.71 | 39.28 (16.07+23.21) |
| Alilia | “li” Njeo ya wakati uliopita(29) | “li” njeo ya wakati (9) | kakosea(18) | 51.79 | 48.21 (16.07+32.14) |

Jedwali Na. 4.7 inaonesha uchambuzi wa lengo la kwanza la utafiti huu, ambalo lilichambua kwa upande wa maumbo ya mofu njeo kwenye hojaji kupitia sampuli ya wanafunzi. Kwahivyo tukianzia na kitendo**Ninakwenda** ambayo “ni” njeo ya wakati unaoendelea, watafitiwa 43 walijibu kwa usahihi ambao sawa na 76.78%, ama

watafitiwa4 tu sawa 7.14% ndio waliojaribu na watafitiwa9 ambao ni 16.07% wamekosea kabisa uchambuzi wa mofu njeo. Matokeo yanaonesha kwamba wanafunzi wengi wanaelewa njeo za wakati unaoendelea, ingawa wapo wanafunzi wachache ambao hawaelewi njeo hizi kabisa.

Kitendo **Mtaimba** kimeonekana kwamba watafitiwa 4 tu ndio waliojibu kwa usahihi ambao ni 7.14%, watafitiwa 29 sawa na 51.79% walijaribu, na watafitiwa 23 sawa na 41.07% walikosea. Kutokana na takwimu hii inaonesha kwamba wanafunzi wachache ndio wanaoweza kuchambua kwa usahihi mofu njeo za wakati unaokuja, hata hivyowanafunzi wengi wameshindwa kuchambua njeo za wakati ujao.

Tukiangalia kitendo **Unaimba** katika jedwali 4.10 hapo juu inaonesha kwamba watafitiwa31 wamejibu kwa usahihi ambao ni sawa na 55,35%, watafitiwa 14 ambao ni 25% wamejaribu na watafitiwa 11 walikosea ambao ni sawa na asilimia 19.64%. Hapa inaonekana wazi kwamba wanafunzi wengi wanaelewa njeo za wakati unaoendelea.

Katika kitendo **Tunakwenda** tunawaona watafitiwa34 sawa na 60.71% wamejibu kwa usahihi, watafitiwa6wamejaribu sawa na 10.71% na watafitiwa 16 wamekosea ambao sawa na 28.55%. Hivyo matokeo ya kitendo hiki yanaonesha kuwa njeo za wakati unaondelea wanafunzi wengi wanaelewa uchambuzi wake kwa kina, ingawa kuna wanafunzi wachache ambao hawazielewi.

Kitendo **Watalia** watafitiwa 34 ambao ni sawa na 60.71% walijibu kwa usahihi, watafitiwa 9 ambao sawa 16.07% walijaribu na watafitiwa 13 sawa na 23.21%

walikosea, mtafiti aliona kwamba wingi wa wanafunzi wanaelewa njeo za wakati ujao, ingawa wapo wachache ambao hawaelewi uchambuzi wa njeo hizi, kama tunavyoona katika jedwali 4.10 hapo juu.

Watafitiwa 29 sawa 51.79% waliojibu kwenye kitenzi **Alilia,** walionesha uwelewa wa kitendo hichi kilichopita, watafitiwa 9 sawa na 16.07% walijaribu, na watafitiwa 18 sawa na 32.14% walikosea kuchambua njeo za wakati uliopita. Matokeo ya swali hili mtafiti aligundua kuwa licha ya wanafunzi wa kidato cha pili kushindwa kuchambua kitendo cha wakati uliopita, lakiniwapo waliojaribu ambao hawakukamilisha uchambuzi huo.

Mfano sahihi wa mofu njeo katika kitendo **“Alilia**”

| | |
|---|---|
| “Li” inaonesha wakati uliopita. | Jibu sahihi |
| “Li” inaonesha wakati. | Amejaribu |
| “Li” inaonesha wakati ujao. | Amekosea |

Mifano hii inadhihirisha kiwango cha umahiri wa uchambuzi wa wanafunzi katika mofu njeo katika vitenzi vya Kiswahili. Uchambuzi huu umetoa mwelekeo wa kiwango cha wanafunzi katika uwezo wao wa kuchambua mofu njeo katika lugha ya Kiswahili. Majumuisho ya hoja hii yanatoa tathmini ya kuwa wanafunzi wapo katika kiwango cha wastani wa 52.02% katika suali la uchambuzi wa mofu njeo. Hoja hii inatokana na uchambuzi wa takwimu za hapo juu pamoja na kuthibitishwa na misingi ya nadharia ya mofofonolojia inayozingatia kuwa umahiri wa wanafunzi katika mofolojia unatoakana na uwezo mzuri wa kuchambua muundo wa mofimu katika lugha pamoja na kuchunguza mabadiliko ya sauti yanayojitokeza katika maneno ili kuunda mofu katika neno hilo kutokana na mofimu ya aina moja. Hivyo

utafiti ulijumuisha na kubaini kwamba wanafunzi wanauwelewa wa kiwango cha wastani katika uchambuzi wa mofu njeo.

Matokeo ya lengo la kwanza juu ya kiwango cha uelewa wa maumbo ya mofu nafsi na njeo katika Kiswahili Sanifu ni cha wastani wa 56.25% katika uchambuzi wa mofu nafsi na 52.08% katika uchambuzi wa mofu njeo. Hali hii imesababishwa na changamoto mbalimbali zinaziochangia baadhi ya wanafunzi kushindwa kuchambua maumbo haya ya mofu nafsi na njeo kwa usahihi. Changamoto hizo zimejadiliwa kwa kina katika lengo la pili la utafiti huu kama zinavyooonekana hapo chini.

### 4.3 Changamoto za Ujifunzaji na Ufundishaji wa Mada ya Mofu

Lengo la pili la utafiti huu ni kubainisha changamoto za ujifunzaji na ufundishaji wa mofu nafsi na njeo za Kiswahili Sanifu kwa shule za Zanzibar.Katika kufikia lengo hili mtafiti alitumia njia ya usaili kwa walimu pamoja na hojaji kwa sampuli ya wanafunzi. Data zilizopatikana katika lengo hili zilichambuliwa kwa kutumia misingi ya nadharia ya linganuzi. Utafiti ulibaini kuwa katika kujifunza/ kufundisha kipengele cha mofu nafsi na njeo hujitokeza changamoto mbalimbali katika uchanganuzi wa vitenzi. Miongoni mwa changamoto zilizojitokeza kwa wanafunzi wa wanapojifunza na walimu wanapofundisha mada ya mofu nafsi na njeo za Kiswahili zinzonekana jinsi zilivyochambuliwahapo chini.

#### 4.3.1 Uwasilishaji wa Data

Kipengele hiki kimechambua taarifa zilizopatikana kupitia njia ya usaili na hojaji, taarifa hizi zinahusiana na changamoto za kujifunza na kufundisha mada ya mofu na nafsi njeo. Kwa kupitia njia ya usaili mtafiti alibaini idadi ya walimu waliopatiwa

miongozo au mafunzo mbalimbali pamoja na aina ya miongozo hiyo. Sambamba na hilo mtafiti kupitia njia ya hojaji, ilimsaidia kupata taarifa zinazohusiana na changamoto za kujifunza mada ya mofu nafsi na njeo. Uchambuzi wa kina wa taarifa hizo kama unavyoonekana hapo chini.

#### 4.3.1.1 Walimu Waliopatiwa Muongozo/Mafunzo ya Mada ya Mofu

Muongozo au mafunzo ya ufundishaji ni jambo muhimu sana katika suali la ufundishaji. Mtafiti alitaka kuona ni kwa asilimia ngapi walimu wa somo la Kiswahili wanafundisha mada kwa kutumia miongozo au mafunzo stahiki kwenye mada husika, 75% ya walimu walikiri kupatiwa na kuitumia miongozo na mafunzo ya mada hii, kama inavyoonesha katika jedwali Na.4.8 hapo chini.

**Jedwali Na. 4.8 Walimu Waliopatiwa Muongozo / Mafunzo ya Mada ya Mofu**


| | Idadi | **%** |
|---|---|---|
| Ndiyo | 18 | 75 |
| Hapana | 6 | 25 |
| **Jumla** | **24** | **100** |

Kutokana na jedwali Na. 4.8 hapo juu tunaona kwamba 75% ya wahojiwa ni walimu waliopatiwa muongozo au mafunzo katika mada ya mofu, na 25% ni walimu ambao hawakubahatika kupatiwa muongozo au mafunzo ya mada hii. Moja kati ya sababu ya baadhi ya wanafunzi kushindwa kuchambu maumbo ya mofu nafsi na njeo, ni walimu kutokupatiwa miongozo au mafunzo ya ufundishaji juu ya mada ya mofu. Kutokana na matokeo hayo mtafiti ameona kwamba ni vyema mafunzo yatolewe

kwa walimu wote wanaofundisha Kiswahili, dai hii limefafanuliwa vizuri na Downing (1969) kwa kusema kuwa ili kuepukana na dhana potofu kuhusu uandishi ni vyema kueka miongozo itakayotoa mawazo na ufundi wa lugha husika, hivyo kutoka na kauli hii, walimu wanaposomesha mada ya mofu inawapasa watumie miongozo au mafunzo waliyoyapata juu ya mada ya mofu, pamoja na kufatilia mada ambazo wanazifundishaili uengezeke ufanisi katika ufundishaji wa mada ya mofu/mofimu.

#### 4.3.1.2 Aina za Miongozo/Mafunzo Katika Kufundisha Mada ya Mofu

Imejitokeza kwenye utafiti huu kwamba kwenye shule zote zilizofanyiwa utafiti, kuna vifaa, miongozo, vitabu pamoja na vifaa vya kisasa ambavyo ni santuri ya sauti na ya picha (CD na DVD) ambavyo hutumika katika uchambuzi wa mofu, kama inavyoonekana kwenye chati Na.4.2 kama hivi ifuatavyo:




**Chati Na.4.2 Aina za Miongozo/Mafunzo Katika Ufundishaji Mada ya Mofu**

Matokeo katika swali hili yalionekana kwamba walimu 16 sawa 67% ndio waliotumia Vitabu, Makala pamoja na santuri ya sauti na ya picha (CD na DVD). Walimu 5 sawa na 21% walitumia vitabu na makala, walimu 3 ambao ni sawa na 12% wamebainika kuwa wanasomesha bila ya kupatiwa miongozo au vifaa katika ufundishaji. Kutokana na matokeo haya mtafiti alibaini kwamba walimu wengi hutumia vitabu, makala na vifaa vya kisasa yaani santuri ya sauti na ya picha wakati wa kufundisha mada ya mofu. Hivyo mtafiti anapendekeza kuwa ni vyema walimu wachanganye miongozo tofauti wakati wakifundisha ili kupata ufanisi mzuri katika uchambuzi wa mada hii ya mofu. Ingawa 12%ya walimu hawatumii miongozo wala vifaa/zana yoyote katika ufundishaji, hali hii ni dalili tosha ya mwelekeo usio mzuri katika ufundishaji,hoja hii inapendekezwa kuwa katika ufundishaji wa stadi ya mazungumzo, walimu watumie zana mbali mbali katika ufundishaji (ZMRC, 2010). kwa hali hivyo utaratibu na mpango madhubuti upangwe ili walimu watumie vifaa wakati wa kufundisha, na isiwe kwa ufundishaji wa stadi za mazungumzo tu pia vifaa vitumike kwa ufundishaji wa mada ya mofu.

## 4.3 Changamoto Katika Kujifunza na Kufundisha Mada ya Mofu

Kipengele hiki kimefafanua juu ya changamoto mbali mbali zinazojitokeza katika mchakato wa kufundisha na kujifunza uchambuzi wa mofu nafsi na njeo, utafiti ulibaini kuwa zipo changamoto zinazowakabili walimu katika kufundisha na kuainishwa kama ni changamoto za kufundisha, na zipo changamoto zinazowakabili wanafunzi katika kujifunza na kuainishwa kama ni changamoto za kujifunza. Ufafanuzi huo ni kama ulivyofafanuliwa hapo chini katika majedwali Na. 4.9 na 4.10.

**Jedwali Na.4.9 Changamoto za Ufundishaji wa Mofu Nafsi na Njeo**

| **Na.** | **Aina ya Changamoto** | **walio kubali** | | **walio kataa** | | **wasio na uhakika** | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Idadi | % | Idadi | % | Idadi | % |
| 1 | Uhaba wa vitabu vya kufundishia Kiswahili mashuleni. | 18 | 75.00 | 6 | 25.00 | 0 | 0 |
| 2 | Somo la Kiswahili hupangiwa walimu wasiowataalamu. | 10 | 41.67 | 12 | 50.00 | 2 | 8.33 |
| 3 | Idadi kubwa ya wanafunzi madarasani. | 19 | 79.17 | 4 | 16.67 | 1 | 4.17 |
| 4 | Baadhi ya waalimu kutokuwa na uwelewa mzuri wa mada ya mofu. | 6 | 25 | 15 | 62.5 | 3 | 12.50 |
| 5 | Utoro wa wanafunzi madarasani. | 20 | 83.33 | 0 | 0 | 4 | 16.67 |

#### 4.3.3.1 Changamoto Katika Ufundishaji wa Mada ya Mofu kwa walimu

Utafiti umebaini kuwa walimu wengi katika skuli teule za Zanzibar wanapambana na changamoto nyingi katika mchakato wa kufundisha mada ya mofolojia hususani katika kipengele cha uchambuzi wa mofu. Miongoni mwa changamoto hizo ni:

**a) Uchache wa Vitabu Rejea vya Kufundishia**

Utafiti umebaini kuwa upungufu wa vitabu rejea ni changamoto kubwa iliyoonekana kwa walimu. Changamoto hii ilionekana wazi kutokana data zilizokusanywakupitia usali wa walimu. Walimu walitoa maoni yao iwapo wamekubaliana na hoja, wamekataa au kutokua na uhakikai, kama inavyoonekana katika jedwali Na. 4.12 hapo juu, watafitiwa 18 sawa 75% kwa sampuli ya walimu inaonekana kuwa walikubali kuwa hoja hii ni changamoto kubwa katika kufundisha. Watafitiwa 6 sawa 25% walikataa na hakujitokeza mtafitiwa ambae hakuwa na uhakika juu ya hoja hii. Hoja hii inathibitishwa na msingi wa nadharia ya linganuzi unaoeleza kuwa; huonekana matatizo katika kuchanganua lugha kwa kuchambua muundo na maumbo yake, msingi huu unakubaliana na hoja hii kwa sababu ikiwa shule hakuna rejea za kutosha mwalimu hatokuwa na wezi wa kufundisha kwa ufanisi. Kwa mantiki hiyo, vitabu na miongozo ni umuhimu katika kufanikisha dhana ya ufundishaji. Dai hili linaungwa mkono na mtafiti ndossi (2001) kwa kusema kwamba kutokupatiwa vitabu ama miongozo ya kutosha ni chanzo kikubwa cha tatizo la uandishi, hasa kwa lugha ya Kiswahili katika ngazi za, namtafiti anaungana na hoja hiyo kwakuona kwamba uhaba wa vitabu vya kufundishia na vya kujifuzia ni changamoto kubwa ambayo inasababisha walimu kutokufundisha kwa ufanisi zaidi.

**b) Somo la Kiswahili Kupangiwa Walimu Wasio Wataalamu**

Mwitikio wa hoja hiyo unaonekana katika jedwali Na. 4.12 hapo juu, ambao watafitiwa 10 sawa na 41.67% walikubali hoja kuwa walimu kupangiwa somo la Kiswahili ikiwa sio wataalamu kuwa ni changamoto, watafitiwa 12 sawa na 50.00% walikataa na watafitiwa 2 sawa na 8.33% hawakuwa na uhakika na hoja hiyo.

Matokeo katika hoja hii yameonesha kwamba ikiwa mwalimu anasomesha Kiswahili lakini sio mtaalamu wa somo la Kiswahili yaani siyo kada yake aliyosomea, inaonekana kuwa ni changamoto kubwa juu ya ufundishaji wake hasa katika mada ya mofu kwenye uchambuzi wa vitendo mbalimbali. Takwimu hizi zinatiliwa nguvu na msingi wa nadharia ya linganuzi unaoeleza kuwa lugha ina ugumu na changamoto zake katika kujifunza na hasa ikiwa ni lugha ya pili. Msingi huu unamaana kuwa siku zote kujifunza lugha ambayo si lugha mama inakuwa na ugumu na matatizo yake. Hivyo utafiti huu unathibitisha kuwa mwalimu kupangiwa somo la Kiswahili bila ya kusomea somo hilo ni changamoto katika ufundishaji, na hasa katika mada ya mofu kwenyevipengele vya nafsi na njeo  kama changamoto hizo zilivyojitokea kwa watafitiwa ambao ni walimu na wanafunzi kama alivybainisha  mtafiki hapo awali.

**c) Idadi Kubwa ya Wanafunzi Madarasani**

Mtafiti alitaka kujua kwamba idadi kubwa ya wanafunzi madarasani kuwa ni changamoto au sio changamoto katika ufundishaji, kwa kuwataka watafitiwa kujibu kwakuchagua kujibu kuwa ni kweli, sio kweli au kama hana uhakika juu ha hoja hiyo.

Utafiti ulibaini kuwa idadi kubwa ya wanafunzi madarasani ni miongoni mwa changamoto katika ufundishaji wa lugha ya Kiswahili hasa katika mada ya mofu. Hoja hii ilithibitishwa kupitia usaili waliofanyiwa walimu, ambao watafitiwa 19 sawa na 79.17% walikubali kuwa idadi kubwa ya wanafunzi ni changamoto katika ufundishaji. Watafitiwa 4 sawa 16.67% walikataa, na mtafitiwa 1 sawa 4.17% hakuwa na uhakika. Katika hali ya kawaida mwalimu anatakiwa anapofundisha aweze kulidhibiti darasa lote ili aweze kutathmini kwa kila kipengele

alichokifundisha, kwa lengo la kupima kila ufahamu wa wanafunzi. hoja hii imetiliwa mkazo na msingi wa nadharia ya Linganuzi kama unavyoeleza kwa kusema kuwa "Lugha ina ugumu na changamoto zake katika kujifunza na hasa ikiwa ni lugha ya pili." Hali hii ina maana kuwa ikiwa mwalimu atashindwa kulidhibiti darasa kulingana na idadi kubwa wa wanafunzi, wanafunzi hawa watashindwa kujifunza lugha kwa ufanisi ukizingatia na hasa ikiwa Kiswahili Sanifu sio lugha yao mama. Kutokana na matokeo hayo mtafiti alithibitisha kuwa idadi kubwa ya wanafunzi madarasani inachangia kwa kiasi kikubwa walimu kutokuwa na udhibiti mzuri wa wanafunzi wao, na kusababisha ugumu katika kufundisha mada mbali mbali mojawapo ikiwa ni mada ya mofu.

**d) Baadhi ya Walimu Kutokuwa na Uwelewa Mzuri wa Mada ya Mofu**

Utafiti umebaini kuwa walimu kutokuwa na uelewa mzuri wa mada ya mofu ni changamoto kubwa katika ufundishaji wa mada hii. Hoja hii imethibitika kutokana na idadi kubwa ya watafitiwa kuthibitisha hali hiyo kupitia usaili. Utafiti uliwasaili watafitiwa 24 katika sampuli ya walimu ambao waliojibu swali hili walikuwa na majibu yafuatayo; watafitiwa 6 sawa na 25% wamekubali hoja hii kuwa walimu kutokuwa na uelewa mzuri wa mada ni changamoto katika ufundishaji wa mada hii. Watafitiwa 15 sawa 62.5% hawakukubaliana na hoja hii na watafitiwa 3 sawa na 12.5% hawana uhakika. Hivyo matokeo ya hoja hii yanaonesha kuwa asilimia kubwa ya walimu hawakukubaliana na hoja hii moja kwa moja kwa madai ya kuwa ikiwa mwalimu atafanya juhudi ya kufuatilia mada hii haiwezi kuwa kikwanzo katika ufundishaji. Nadharia ya linganuzi inakubaliana na sampuli ya watu sita waliokubali kuwa uelewa mdogo wa walimu katika mada ya mofu ni changamoto katika

kufundisha mada hii, kwa sababu kawaida kuna matatizo katika kuchanganua lugha kwa kuchambua muundo na maumbo yake. Hivyo utafiti huu unakubaliana na hoja hii kuwa miongoni mwa changamoto katika ufundishaji wa mada ya mofu ni mwalimu kutokuwa na uelewa juu ya mada hii.

**e) Utoro wa Wanafunzi Madarasani**

Utafiti ulibaini kuwa suala la utoro wa wanafunzi, kukimbia marasani na shule kwa ujumla ni miongoni mwa changamoto katika ufundishaji wa lugha ya Kiswahili hasa katika mada ya mofu. Hoja hii ilithibitishwa kupitia usaili waliofanyiwa walimu, ambapo watafitiwa 20 sawa na 83.33% walikubaliana na hoja ya utoro kama ni changamoto ya ufundishaji lugha ya Kiswahili, hakujitokeza mtafitiwa aliekataa nawatafitiwa 4 sawa na 16.67% hawakuwa na uhakika kwamba utoro wa wanafunzi ni miongoni mwa changamoto katika kujifunza mada ya mofu. Tafsiri ya matokeo haya yanaonesha kuwa utoro wa wanafunzi ambao hawahudhurii vipindi darasani ni changamoto kubwa katika mada ya mofu kwavile wanafunzi hushindwakuelewa muendelezo mzima wa uchambuzi wa mofu katika vitenzi, hoja hii pia inathitishwa na Ndossi (2001) yeye alichunguza matatizo ya uandishi kwa shule za Tanzania, kwa kusema kuwa "*endapo mahurio darasani yatakuwa mabaya, ni dhahiri kuwa mwanafunzi hatoweza kupata taaluma ya kutosha itakayomsaidia kumudu stadi ya uandishimzuri na taratibu zake".* Suala la utoro wa wanafunzi ni changamoto kama ambavyo msingi wa nadharia ya Linganuzi unavyoeleza kwa kusema kuwa "Lugha ya Kiswahili ina ugumu na changamoto zake katika kujifunza hasa ikiwa ni lugha ya pili." Hali hii ina maana kuwa kama mwanafunzi hahudhurii shule ipasavyo na hivyo hapati uzoefu wa kutosha wa kuweza kujifunza na hasa katika uchambuzi wa mofu.

Kwa hivyo ni wazi kuwa utoro ni suali ambalo husababisha wanafunzi kukosa taaluma na uweledi ambao angeutumia katika kujifunza masomo yake hususan kwenye mada ya maumbo ya mofu nafsi na njeo.

**Jedwali Na. 4.10 Changamoto za Ujifunzaji kwa Wanafunzi**

| **Na.** | **Aina za Changamoto** | **walio kubali** | | **walio kataa** | | **wasio na uhakika** | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Idadi | % | Idadi | % | Idadi | % |
| 1 | Uhaba wa vitabu vya kujifunzia Kiswahili mashuleni | 51 | 91.07 | 5 | 8.93 | 0 | 0 |
| 2 | Mwamko mdogo kuhusu somo la Kiswahili kwa wanafunzi. | 30 | 53.57 | 15 | 26.79 | 11 | 19.64 |
| 3 | Wanafunzi kushindwa kuelewa aina za maneno na kupelekea ugumu wa kuchanganua viambishi vya nafsi na njeo. | 37 | 66.07 | 13 | 23.21 | 6 | 10.71 |
| 4 | Wanafunzi wanashindwa kutofautisha kati ya mofu na mofimu | 44 | 78.57 | 7 | 12.50 | 5 | 8.93 |
| 5 | Ugumu wa mada kulingana na kiwango cha elimu kwa wanafunzi | 35 | 62.50 | 5 | 8.93 | 16 | 28.57 |

### 4.3.2.2 Changamoto Katika Kujifunza Mofu Nafsi na Njeo kwa wanafunzi

Utafiti umebaini kuwa wanafunzi katika shule teule wanapambana na changamoto nyingi katika mchakato wa uchambuzi wa maumbo ya mofu hasa kwenye nafsi na njeo za Kiswahili sanifu. Miongoni mwa changamoto hizo ni:

**a) Uchache wa Vitabu Rejea vya Kujifunzia**

Utafiti umebaini kuwa upungufu wa vitabu rejea ni changamoto kubwa iliyoonekana kwa wanafunzi. Changamoto hii ilionekana wazi kutokana data zilizokusanywa katika hojaji. Wanafunzi walitoa maoni yao iwapo wamekubaliana na hoja,wamekataa au kutokuwa na uhakika, kama inavyoonekana katika jedwali Na.4.13 hapo juu, Tukiangalia data za wanafunzi tunaona kwamba watafitiwa 51 sawa na 91.07% wamekukubali, watafitiwa 5 sawa na 8.93% walikataa, pia hakukua na mtafitiwa asiekua na uhakika. Hoja hii inathibitishwa na msingi wa nadharia ya linganuzi unaoeleza kuwa; huonekana matatizo katika kuchanganua lugha kwa kuchambua muundo na maumbo yake. Msingi huu unakubaliana na hoja hii kwa sababu pindipo shuleni kuna uhaba wa rejea, wanafunzi watashindwa kujenga kumbukumbu ya kutosha juu ya anachojifunza na kushindwa kupata mbinu bora za kujifunza uchambuzi wa mofu njeo na nafsi. Kutokana na hayo inaonekana kwamba vitabu na miongozo ni muhimu katika kufanikisha dhana ya kujifunza. Dai hili linaungwa mkono na mtafiti ndossi (2001) kwa na kusema kwamba kutokupatiwa vitabu ama miongozo ya kutosha ni chanzo kikubwa cha tatizo la uandishi, hasa kwa lugha ya Kiswahili, mtafiti anaungana na hoja hiyo kwa vile uhaba wa vitabu vya kujifuzia ni changamoto kubwa ambayo inasababisha wanafunzi kutokujifunza kwa umakini.

**a) Mwamko Mdogo wa Somo la Kiswahili kwa Wanafunzi**

Utafiti umebaini kuwa muamko mdogo wa somo la Kiswahili kwa wanafunzi ni changamoto kwa walimu katika ufundishaji na wanafunzi wenyewe katika mchakato wa kujifunza. Hoja hii imethibitika kutokana na idadi kubwa ya watafitiwa kuthibitisha hali hiyo kupitia usaili. Utafiti ulibaini kuwa watafitiwa khamsini na sita (56) waliojibu swali hili walikuwa na majibu yafuatayo; watafitiwa 30 sawa na 53.57% wamekubali kuwa suali la muamko mdogo wa somo la kiswahili ni changamoto katika kujifunza lugha ya Kiswahili. Watafitiwa 15 sawa na 29.79% wamekataa na watafitiwa 11 sawa 19.64% hawakuwa na uhakika. Takwimu hizi zikifafanuliwa na msingi wa nadharia ya Linganuzi unaosema kuwa "Lugha ina ugumu na changamoto zake katika kujifunza na hasa ikiwa ni lugha ya pili." Msingi huu unamaana kuwa kujifunza lugha ambayo sio lugha mama kuna ugumu na changamoto zake hasa kwa mwanafunzi ambaye hana muamko katika kujifunza somo la Kiswahili. Kwa hiyo mtafiti alibaini kwamba wanafunzi wasio na muamko katika somo la Kiswahili ni changamoto inayowakumba walimu katika kufundisha na wanafunzi wenyewe katika kujifunza.Hivyo walimu wawape motisha wanafunzi juu ya mada ya mofu, kwani motisha ni moja wapo ya mbinu inayochangia mwanafunzi kujifunza vizuri (Mbunda, 1979). Kwa hivyo wanafunzi wanaweza kuwa na mwamko wa kujifunza kutokana na kupewa motisha katika somo la Kiswahili.

**b) Kushindwa Kuelewa Aina za Maneno**

Utafiti ulibanini kuwa miongoni mwa changamato katika suala la uchambuzi wa mofu katika vitenzi vya Kiswahili ni pamoja na wanafunzi kushindwa kuelewa aina

za maneno, hali ambayo inasababisha ugumu wa kuchambua mofu za nafsi na njeo katika vitendovya lugha ya Kiswahili. Hali hii imethibitika kutokana na watafitiwa 37 kati ya watafitiwa 56 waliojibu swali hili ambao ni sawa na 66.06% walikubaliana na hoja hii, 13 sawa na 23.21% walikataa hoja hii na 6 ambao sawa 10.71% hawakuwa na uhakika juu ya hoja hii. Hoja hii inathibitishwa na msingi wa nadharia ya Linganuzi unaoeleza kuwa; kuna matatizo katika kuchanganua lugha katika muundo na maumbo yake, msingi huu unamaana kuwa wanafunzi wengi wanashindwa kuchanganua muundo na maumbo ya lugha kutokana na kuathiriwa na lugha mama kama vile lahaja yake ya asili au lugha yake ya kwanza. Hivyo mtafiti alibaini kwamba wanafunzi kutokuelewa aina za maneno ni changamoto inayochangia kupata ugumu wakati wa uchambuzi wa maumbo ya mofu nafsi na njeo katika Kiswahili Sanifu.

**c) Kushindwa Kutofautisha Kati ya Mofu na Mofimu**

Utafiti ulibaini kwamba wanafunzi kushindwa kutafautisha kati ya mofu na mofimu ni changamoto kubwa katika ujifunzaji wa mada ya mofu kwa wanafunzi. Hoja hii inathibitika kutokana na watafitiwa 44 kati ya watafitiwa 56 waliojibu swali hili ambao ni sawa na 78.57% wamekubali kuwa hoja hii ni changamoto katika ujifunzaji kwa wanafunzi, 7 sawa na 12.5% walikataa hoja hii na 5 sawa na 8.929% hawakuwa na uhakika katika hoja hii. Hoja hii inathibitishwa na msingi wa nadharia ya Linganuzi unaoeleza kuwa; kuna matatizo katika kuchanganua lugha kwa kuchambua muundo na maumbo yake. Msingi huu unakubaliana na hoja hii kwa sababu ikiwa mwalimu atashindwa kutofautisha mofu na mofimu ni lazima mwanafunzi naye atashindwa kutofautisha dhana hizo kutokana na wanafunzi kufata

wanachoelekezwa na walimu wao.Hali hii husababisha mwanafunzi kushindwa kupata motisha na mbinu bora za kujifunza uchambuzi wa mofu njeo na nafsi. Kwa hivyo utafiti huu kutokana na takwimu ya hapo juu unathibitisha kuwa suala la wanafunzi kushindwa kutofautisha kati ya mofu na mofimu ni changamoto kubwa kwa wanafunzi wenyewe katika kujifunza. Hata hivyo utafiti umebaini kuwa wanafunzi wanadhana kuwa mofu na mofimu ni dhana moja na zinabeba dhima moja katika uchambuzi wa maneno katika lugha ya Kiswahili. Dhana hii si sahihi kama inavyothibitishwa na Habwe na Karanja (kesh), anafasili kwa kusema kuwa uhusiano kati ya mofu na mofimu ni ule wa umbo na yaliyomo au kiashiria na kiashiriwa.

Kwamfano (a) – (na) – (pik) – (a)

Mofu (–a-) huwa na mofimu zifuatazo:

i. Mtenda
ii. Nafsi ya tatu umoja
iii. Kiambishi kipatanishi cha kisarufi cha ngeli ya kwanza

Kwa hivyo mofu inaweza ikawa moja na mofimu zikawa zaidi ya moja.

**d) Ugumu wa Mada Kulingana na Kiwango cha Wanafunzi**

Utafiti ulibaini kuwa miongoni mwa changamoto katika kujifunza mofu njeo na nafsi ni suala la ugumu wa mada ya mofu kulingana na kiwango chao cha elimu kwa wanafunzi wa kidato cha pili. Mada ya mofu inaanza kusomwa kuanzia kidato cha pili kwa kiwango hiki utafiti ulibini kuwa wanafunzi wengi wanashindwa kujifunza kwa ufanisi mada hii kulingana na kiwango hiki cha elimu. Hoja hii imethibitika kutokana na takwimu zilizokusanywa katika utafiti huu. Kwa vile watafitiwa 35 kati ya watafitiwa 56 ambao ni sawa na 62.50% kukubali hoja hii kuwa ugumu wa mada

kulingana na kiwango cha wanafunzi ni changamoto katika kujifunza uchambuzi wa maumbo ya mofu. Watafitiwa 5 sawa na 8.93% walikataa hoja hii na watafitiwa 16 sawa na 28.57% hawakuwa na uhakika juu ya hoja hii. Kutokana na matokeo hayo mtafiti alibaini kwamba ugumu wa mada kutokana na kiwango cha wanafunzi ni changamoto kubwa inayowakumba wanafunzi, na uthibitisho wa hoja hiiinadhihirika pale BLMT (2016) lilipochambua swali lililomtaka mtahiniwa kueleza dhamira za mofimu ***li,*** kama ilivyotumika katika sentensi tano alizopewa. Matokeo ya swali hili linaonekana kuwa swali hilo ni miongoni mwa maswali yaliyojibiwa vibaya sana na watahiniwa wengi kwavile 93.1% ya watahiniwa kushindwa kueleza dhima za mofimi ***li***na kupata alama ya 0hadi 1.

## 4.4 Muhtasari wa Sura

Sura ya nne imewasilisha na kuchambua data za utafiti zilizokusanywa kwa njia ya usaili na hojaji. Data zilizokusanywa zilichambuliwa kwa kutumia nadharia mbili; nadharia ya mofofonolojia na nadhiria linganuzi. Matokeo yaliyopatikana yamewasilishwa kwa kugaiwa katika sehemu kuu mbili kulingana na malengo ya utafiti huu. Sehemu ya kwanza imechambua taarifa za lengo la kwanza linaloeleza juu ya kuainisha kiwango cha uelewa wa maumbo ya mofu nafsi na njeo katika Kiswahili Sanifu kwa wanafunzi wa Zanzibar na sehemu ya pili ilijikita na uchambuzi wa taarifa zinazohusu lengo la pili linalohitaji kubainisha changamoto za ujifunzaji na ufundishaji wa mofu nafsi na njeo za Kiswahili Sanifu katika shule za Zanzibar. Matokeo ya lengo la kwanza juu ya kiwango cha uelewa wa maumbo ya mofu nafsi na njeo katika Kiswahili Sanifu ni cha wastani wa 56.25% katika uchambuzi wa mofu nafsi na 52.08% katika uchambuzi wa mofu njeo. Ama kwa

upande wa lengo la pili lililoshuhulika katika kubainisha changamoto za ujifunzaji na ufundishaji wa mofu nafsi na njeo za Kiswahili sanifu.Matokeo ya swali hili inaonekana kuwa zipo changamoto nyingi za ujifunzaji na ufundishaji miongoni baadhi yake ni;

1dadi kubwa ya wanafunzi madarasani, baadhi ya walimu kutokuwa na uwelewa mzuri wa mada ya mofu, baadhi ya walimu kutokupata mafunzo ya ufundishaji mada ya mofu,Uhaba wa vitabu vya kujifunzia na kufundishia Kiswahili mashuleni, utoro wa wanafunzi madarasani namwamko mdogo kuhusu somo la Kiswahili kwa wanafunzi.

Kutokana changamoto hizo ambazo zilijadiliwa na walimu katika usaili na wanafunzi kupitia hojaji, inaonekana kwamba ni kikwazo kikubwa kwa walimu katika swali zima la ufundishaji, halkadhali wanafunzi pia wanakwazwa katika swali la kujifunza. Hivyo mtafiti alibaini kuwa suluhisho la changamoto hizokatika mada ya mofu nafsi na njeo ni pamoja na kuwepo kwa marejeo ya kutosha kwa walimu pamojana wanafunziili walimu wafundishe kwa ufanisi zaidi na wanafunzi wajifunze kwa kujiamini na kupata kumbukumbu za muda mrefu. Pamoja na hayo walimu wapatiwe miongozo na mafunzo ya mara kwa mara yanayohusiana na mada ya mofu ili wafundishe kwa uweledizaidi. Pia wanafunzi wapewe mazoezi ya kutosha na endelevu ya mara kwa mara yanayohusiana na uchambuzi wa maumbo ya mofu nafsi na njeo za Kiswahili sanifu.

# SURA YA TANO

# MUHUTASARI WA UTAFITI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

## 5.1 Muhutasari wa Utafiti

Utafiti huu ulikua na lengo la kupima uwelewa wa matumizi ya mofu nafsi na njeo kwa wanafunzi wa Zanzibar. Walengwa walioshiriki kwa ujumla kwa kujaza hojaji na kusailiwa walikuwa 80, kati yao 56 ni sampuli ya wanafunzi na 24 ni sampuli ya walimu.Watafitiwa waliohusika walitoka katika shule mbali mbali za Zanzibar, ambazo ni shule ya ya Chumbuni, shule ya Vikokotoni, shule ya ya Bububu na shule ya ya Mtopepo.

Ili kufikia lengo kuu la utafiti huu la kupima uwelewa wa matumizi ya mofu nafsi na njeo kwa wanafunzi wa Zanzibar, utafiti huu ulikua na malengo mahsusi mawili ambayo ni kwanza, kuainisha kiwango cha uwelewa wa maumbo ya mofu nafsi na njeo katika Kiswahili Sanifu kwa wanafunzi wa Zanzibar. Pili, kubainisha changamoto za ujifunzaji na ufundishaji wa mofu nafsi na njeo za Kiswahili Sanifu katika shule za wa Zanzibar. Katika kufikia malengo haya mtafiti alisaili kwa kutumia maswali aliyoyaandaa kama ni muongozo, pia alitumia hojaji kwa walengwa. Pamoja na hayo katika kuchanganua maumbo ya mofu nafsi na njeo mtafiti alitumia nadharia ya mofofonolojia kwa lengo la kwanza la utafiti wake.Pia alitumia nadharialinganuzi katiaka kuchambua lengo la pili la utafiti wake. Hivyo nadharia hizi ndizo zilitumika kuuongoza utafiti huu katka uchanganuzi mzuri wa maumbo ya mofu nafsi na njeo.

Sambamba na hayo utafiti huu uligaiwa katika sehemu kuu mbili kulingana na malengo ya utafiti huu ni; kuainisha kiwango cha uelewa wa maumbo ya mofu nafsi na njeo katika Kiswahili Sanifu kwa wanafunzi wa Zanzibar, na kubainisha changamoto za ujifunzaji na ufundishaji wa mofu nafsi na njeo za Kiswahili Sanifu katika shule za Zanzibar. Ama katika sura ya tano ya utafiti huu imetoa muhtasari wa utafiti, matokeo ya utafiti, hitimisho na mapendekezo ya tafiti zijazo.

## 5.2 Muhtasari wa Matokeo ya Utafiti

Lengo la kwanzala utafiti huu lilikuwa ni kuainisha kiwango cha uelewa wa maumbo ya mofu nafsi na njeo katika Kiswahili Sanifu kwa wanafunzi wa Zanzibar. Matokeo ya lengo hili lilibainisha kwamba, katika nafsi ya kwanza umoja 80.36% ya wanafunzi ndio waliojibu sahihi, halkadhalika katika nafsi ya pili wingi 83.92% walijibu kwa sahihi, piakwenye nafsi ya pili umoja 33.92%tu ndio walipatia, aidha nafsi ya kwanza wingi 48.21% walijibu sahihi, kwaupande wa nafsi ya tatu wingi 44.64% walijibu sahihi, vile vile katika nafsi ya tatu umoja 46.42% walijibu sahihi. Tukiendelea na swali hili kwa upande wa mofu njeo kwenye wakati unaoendelea 76.78% ya wanafunzi walijibu sahihi, aidha wakati ujao 7.14% walijibu kwa usahihi na wakati unaoendelea 55.35% walijibu sahihi, na katika kitendo chengine cha wakati unaoendelea 60.71% walijibu sahihi, wakati ujao 60.71% walijibu sahihi, na kwenye wakati uliopita 51.79% ndio waliojibu kwa usahihi. Tafsiri yalengo hili inaonesha wazi kuwa wanafunzi wa kidato cha pili wanauwelewa wa wastanikatika uchambuzi na uchanganuzi wa maumbo ya mofu nafsi na njeo katika vitenzi mbalimbali, kutokana na data za hapo juu ambazo mjumuisho wake ni wastani wa

56.25% katika uchambuzi mofu nafsi na wastani wa 52.08% kwenye uchambuzi wa mofu njeo.

Lengo la pili la utafiti huu lilikuwa ni kubainisha changamoto za ujifunzaji na ufundishaji wa mofu nafsi na njeo za Kiswahili Sanifu. Matokeo ya lengohili yalionesha wazi kuwa walimu 16 sawa 67% ndio waliotumia Vitabu, Makala pamoja na santuri ya sauti na ya picha (CD na DVD). Walimu 5 sawa na 21%walitumia vitabu na makala, pia walimu 3 sawa na 12% ambao wanasomesha bila ya kupatiwa vifaa. Hivyo mtafiti alibaini kwamba walimu wengi hutumia vitabu, makala na vifaa vya kisasa wakati wa kufundisha mada ya mofu**.** Takwimu hizi zilidhihirisha kuwepo kwa changamoto katika kujifunza na kufundisha. Changamoto zilizoibuliwa na utafiti huu ni pamoja na uchache wa vitabu rejea, utoro wa wanafunzi madarasani, mwamko mdogo wa somo la Kiswahili kwa wanafunzi, wanafunzi kushindwa kutofautisha kati ya mofu na mofimu, ugumu wa mada kulingana na uwezo wa wanafunzi. Pia somo la Kiswahili kupangiwa mwalimu ambae sio kada yake, idadi kubwa ya wanafunzi madarasani, na baadhi ya walimu kutokuwa na uwelewa mzuri wa mada ya mofu ni miongoni mwa changamoto zilizojitokeza katika kukufundisha na kujifunza mada ya mofu.

### 5.3 Hitimisho

Utafiti huu ulihusu kupima uwelewa wa matumizi ya mofu nafsi na njeo za Kiswahili kwa wanafunzi wa Zanzibar. Kwa jumla utafiti ulibaini kuwa kiwango cha wanafunzi cha uelewa wa uchambuzi wa mofu nafsi na njeo kipo katika hali ya wastani. Hali hii inatokana na ukweli kuwa wanafunzi wengi wanaweza kuchambua mofu nafsi na njeo katika hali za kutaja dhima za msingi za mofu hizo bila ya

kuchambua kwa kina juu ya dhima za ziada ambazo wangepaswa kuzichambua katika uchambuzi huo. Pia wapo wanafunzi ambao hawana uwezo wa kuchambua hata dhima za msingi za mofu nafsi na njeo. Uelewa wa kiwango hiki cha wastani kimetokana na changamoto mbalimbali zinazowakabili walimu na wanafunzi katika kujifunza na kufundishachangamoto hizi ziliibuliwa kutokana na lengo la pili la utafiti huu. Miongoni mwa changamoto hizo ni pamoja na kwanza ni suala la ugumu wa mada kulingana na kiwango cha wanafunzi, uhaba wa rejea katika mada hii, utoro wa wanafunzi, idadi kubwa ya wanafunzi katika darasa, wanafunzi kushindwa kujua aina za maneno pamoja na mwalimu wa kupangiwa somo la Kiswahili wakati sio kada yake aliyosomea. Matokeo yote haya yalitokana na data zilizochambuliwa kupitia nadharia ya mofofonolojia na Linganuzi.

## 5.4 Mapendekezo ya Utafiti

Tasnifu hii imeweka mapendekezo ya aina mbili; mapendekezo kwa ajili ya tafiti fuatishina mapendekezo kwa wadau mbalimbali wa lugha. Mapendekezo haya ni sehemu ya maoni ya mtafiti pamoja na kuonesha mapengo ya utafiti huu, ambayo utafiti mwengine unaweza kufanywa kwa ajili kwa kiziba mapengo hayo.

### 5.4.1 Mapendekezo kwa Tafiti Fuatishi

Utafiti huu umekamilika na kutowa matokeo ambayo yanaonesha kuwa bado kunahitajika uchunguzi zaidi ili kuweza kupima kiwango cha uwelewa wa matumizi ya mofu mbalimbali katika lugha ya Kiswahili Zanzibar. Vile vile ni vyema utafiti kama huu ufanyike kwa wanafunzi wa wa vidato. Sambamba na hilo watafiti wengine wachunguze uwelewa wa maumbo ya mofu mbalimbali kama vile mofu za kauli, mofu rejeshi n.k.

### 5.4.2 Mapendekezo kwa Wadau wa Elimu

Wadau wa elimu wawe na uhusiano wa kutosha kwa walimuna wanafunzi katika kuhamasisha ufundishaji na ujifunzaji wa mada ya mofu kwa kutoa vipeperushi mbalimbali vinavyoonesha uchambuzi na uchanganuzi wa maumbo ya mofu kwa lengo la kuwafanya walimu wawe bora katika ufundishaji, piawawe na mpangilio wa kueka warsha na makongamano ya mara kwa mara ya kitaaluma yanayohusiana na mada ya mofu, kama vile urejeshi, ukanushi na nyinginezo. Pia wadau watoe marejeo ya kutosha yanayohusu uchambuzi na uchanganuzi wa mofu tofauti katika vitenzi mbalimbali.

Kutokana na baadhi ya walimu ambao hawajasomea fani ya Kiswahili na wamekosa miongozo au mafunzo ya ufundishaji, ni vyema walimu hao wapatiwe mafunzo maaluma yanayohusiana na mada ya mofu, ili kuwapa walimu hao mwanga na uweledi katika ufundishajiwa mada ya mofu. Mbali ya hayo taasisi husika inayoshughulikia mitaala ya somo la Kiswahili iandae uchanganuzi maalum ambao utakua ni muongozo kwa mwalimu ili kuweza kufundisha kwa mbinu rafiki.

## MAREJELEO

Ali, L. (2015). "Changamoto na Mbinu za Kiisimu katika Ufundishaji wa Stadi ya Mazungumzo kwa Wanafunzi wa Elimu ya Awali," Tasinifu ya Uzamili ya Chuo kikuu Huria cha Tanzania.

Aswan, A. Abdallah, N. na Abedalazizi, M.(2015). "The Awareness of Morpheme Knowledge for Young Adults Vocabulary Learning Online." *The Malaysian Online Journal of Educational Science*, Malaysian. The University of Malaya Malaysian.

Babbie, E. (1999). *The Basic of social Research,* Belmont: Wadsworth Publishing Company.

Baraza la Mitihani la Tanzania (2016). *Taarifa ya Uchambuzi wa Majibu ya Watahiniwa katika Mtihani wa Kidato cha Nne (CSEE) 2015*. Dar es Salaam: Baraza la Mitihani la Tanzania.

Barno, H. C. (2013). "Muundo wa Kimofo- Sintaksia wa Kitenzi cha Kinandi kwa Mtazamo wa Kitenzi cha Kanuni Finyu (KKF)." *Nordic Journal African Studies 22(4): 213 – 235)*. University of Eastern Africa – Baraton, Kenya.

Cooper, R.L. (1990). *Language Planning and Social Change*. Cambridge: Cambridge University Press.

Downing, J. (1969). *How Children think about Reading: Reading from Process to Practice*. London: Routledge and Kegan Paul in Association with the Open University Press.

Enon, C. J. (1998). *Educational Research and Measurement, Department, of Distance Educational*, Makerere University Uganda. Kampala, Uganda.

Faynan, R. (1998). *The Essential Arabic.* New Delhi: Good word Books.

Haji, A. M. (2015). "Uchunguzi wa Maana za Majina katika Jamii ya Wapemba." Tasinifu ya Uzamili ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Hamadi, S. O. (2011). "Tofauti ya Viambishi Njeo na Hali Mbalimbali kati ya Kipemba na Kiswahili Sanifu." Tasinifu ya Shahada ya Uzamili ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Hassan, H. S. (2016). "Udhihirishaji wa Mofu Zinazowakilisha Nafsi na Njeo Katika Kiswahili: Utafiti linganishi kati ya Kiswahili Sanifu na Lahaja ya Kipemba." Tasinifu ya Shahada Uzamili ya Chuo kikuu huria Tanzania.

Karanja, P. na Habwe, J. (2004). *Misingi ya sarufi ya Kiswahili*. Nairobi: Phoenix Publishers. Ltd.

Khan, A. (2014). *Sequential Presentetion of Gramatical Morphemesin EFL Text book and its Relation with Morpheme Asquisition order*, University of Azada Jammu and Kashmir Pakistan.

Kihore, Y. M. (2003). *Sarufi ya Maumbo ya Kiswahili Sanifu* (SAMIKISA) Dar es Salaam: TUKI.

Kimani, J. (2015). *Uhusiano wa Mbinu za Kufundisha Sarufi na Umilisi wa Mazungumzo ya Wanafunzi wa, Kaunti ndogo ya Thika Magharibi*, Kenya. Chuo Kikuu cha Kenyata.

Kipacha, A. (2002). "Launi za Kiswahili Sanifu na Kiswahili Fasaha kwa Tanzania Bara na Zanzibar."

Kitchin, R. na Tale, N (2000). *Conducting Research into Human Geography: Theory, Methodology and Practice,* UK: Peason Educational Limited.

Kitsao, R. (2015). *Makosa ya Kisarufi katika Insha na Jinsi Yanavyopelekea Matokeo Mabaya ya Mitihani Kata ya Ganze, Kaunti ya Kilifi, Kenya*. Chuo Kikuu cha Pwani Kenya.

Kothari, C. R. (1990). *Research Methodology: Methods and Techniques,* New Delhi: New age International Publishers.

Kothari, C. R. (2008). *Research Methodology: Methods and Techniques,* New Delhi, New Age Intenational Publisher LTD.

Kothari, C. R. (2009).*Research Methodology: Methods and Techniques,* New Delhi: New Age Intenational (P) Ltd.

Kothari, C.R. (2004). *Research Methodology: Method and Technology*, New Delhi: Wiley Eastern.

Lado, R. (1957). *Linguistic Across Cultutres*. Michigan: University of Michigan Press.

Massamba, D.P.B. (2002). *Historia ya Kiswahili: 50BK hadi 1500BK*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Mathooko, P. M. (2004). *Matatizo Yanayoitinga Kiswahili kama Lugha ya Kujifunzia Isimu na Vyuoni Vikuu Nchini Kenya.* Nairobi: Kenyatta University.

Mathooko, P. M. (2007). *Isimu Jamii: Misingi na Nadharia*, Nairobi, Kenya: Njiku Books.

Matinde, R.S. (2012). *Dafina ya Lugha: Isimu na Nadharia*, Mwanza: Mwanza Serengeti Educational Publishers (T) Ltd.

Mazrui, A. M. (1983). *Aspect Marking in Swahili According for Vanation Kiswahili*, Dar es salaam: TUKI.

Mbunda, F. L. (1979). "Student interest in the Teaching and Writing of Composition in Tanzania Sekondary schools." unpublished M.A. thesis, University of Dar es Salaam.

Mohammed, J. (2010). "Matatizo yanayowapata wanafunzi Wa Libya katika Kujifunza Viambishi vya Njeo katika lugha ya Kiswahili," Tasinifu ya Shahada ya Uzamili ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Mohammed, S. A. (2013). "Athari za kiisimu za lahaja ya Kimakunduchi katika Kiswahili Sanifu Kilichotumika Shuleni Makunduchi Zanzibar." Tasinifu ya Shahada ya Uzamili ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Mrayat, A. (2015). “Negative particles and morphemes in Jordan an Arabic Dialets.” *Journal of education and practive*. Vol.6, No.36. Mulah, Al karak, Jordan.

Mtavangu, N. (2008). “Tense and an Aspect in Ikihehe in Occasional Paper in Linguistics No.3” *Nordic Journal of African studies 22(4): 213 – 235 (2013)*.

Mugenda, O. M. & Mugenda, A. G. (2003). *Research Methods: Qualitative and Quantitative Approaches*, Nairobi: Acts Press Kenya.

Nassor, S. (2014). “Mifanyiko ya Kimofolojia ya Vitenzi vya Lahaja ya Kimakunduchi Zanzib.” Tasinifu ya Shahada ya Uzamili ya Chuo Kikuu cha Nairobi.

Ndossi, A. (2011). “Chanzo na Suluhisho la Matatizo ya Uandishi wa Kiswahili katika  za Tanzania.” Tasinifu ya Shahada ya Uzamili ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Nyagah, S. (2016). “Uchanganuzi wa Makosa ya Kifonolojia na Kimofolojia yanayojitokeza katika kazi andishi za wanafunzi wa shule za upili, Tigita, Jimbo la Meru.” Tasinifu ya Shahada ya Uzamili ya Chuo kikuu Nairobi.

Obara, J. (2014). “Uchanganuzi wa Makosa yanayofanywa na Wanafunzi Wazungumzaji wa Lugha ya Ekegusii.” Tasinifu ya Shahada ya Uzamili ya Chuo Kikuu Nairobi.

Pedroza, J. G. (ND). *Analysis on Filipino Language Morpheme*, MAEd Student. Curtin http://www.academia.edu/219645/analysis-on-Filipino-language-morphemeRetrieved 15/10/2017

Prewitt, K. (1980). *Introductory Research Methodology*, East African Application Occasional Papers No. 10 institute for Development Studies University of Nairobi.

Rubanza, Y. (2003). *Sarufi Mtazamo wa Kimuundo*, Dar es Salaam: Chuo Kikuu Huria cha Tazania.

Sengo, T. S. Y. (2009). *Sengo na Fasihi za Kinchi.* Dar es Salaam: AERA.

Sign, K. (2007). *Quantitative Social Research Methods*, India: SEGE Publication.

Trubetzkoy, N. S. (1939/1968). *Principlesof Phonology*, Los Angeles. University of Calfonia Press.

University.http://www.Academia.edu/2196645/Analysis_on_Filipino_Language_morphimes

Uwezo, (2010). Utafiti wa Uwezo wa Watoto Kusoma na Kuhesabu Tanzania. (www. uwezo. Net)

Zanzibar Madrasa Resource Centere, (2010). *Principle Curriculum, Supporting Early.*

# VIAMBATISHO

**Kiambatisho Na. 1: usaili (Mahojiano)**

Muongozo wa Mahojiano kwa walimu wanaofundisha somo la Kiswahili shuleni Zanzibar.

**Maelezo**

Mimi ni mwanafunzi wa shahada ya uzamili (MA KISWAHILI) Chuo Kikuu Huria cha Tanzania. Usailihuu madhumuni yake ni kukusanya data za kupima uelewa wa mofu **nafsi** na **njeo** za Kiswahili Sanifu kwa shule za Zanzibar. Taarifa zitakazokusanywa ni kwa ajili ya taaluma tu, na majibu yako yatakuwa ni siri na yatatunzwa. Tafadhali jibu maswali yafuatayo kwa ufasaha ilituweze kukamilisha kazi yetu.

**SEHEMU A: MAELEZO BINAFSI**

Shule …………………………………………………

1. Jee mwalimu................. ni mwalimu wa soma la Kiswahili?
2. Jinsia: mke [ ], mume [ ]
3. Kiwango cha elimu

   i. Cheti [ ]
   ii. Stashahada [ ]
   iii. Shahada [ ]
   iv. Shahada ya uzamili [ ]
   v. Shahada ya uzamivu [ ]

**SEHEMU B: MAELEZO KUHUSU MOFU NAFSI NA NJEO**

Tafadhali jibu maswali yafuatayo.

1. Mwalimu …………..umesomea fani ya Kiswahili?
2. Una uzoefu wa muda gani katika ufundishaji wa somo la Kiswahili?

   Chini ya mwaka mmoja [ ], miaka 1- 3 [ ], miaka 4- 6 [ ],

   Miaka7 – 9 [ ], miaka 10 na kuendelea [ ]
3. Jee uliwahi kupatiwa miongozo / mafunzo ya ufundishaji wa mada hii ya mofu za Kiswahili?

   Ndio [ ], hapana [ ].

   b) Muongozo upi uliopatiwa kwa kufundishia mada ya mofu kati ya hii?

   i. Vitabu na makala [ ]

   ii. Vitabu, makala, CD na DVD [ ]

   iii. Sikupatiwa [ ]
4. Ikiwa wewe ni mwalimu wa Kiswahili, jee unaridhishwa na uchambuzi wa mofu nafsi na njeo kwa wanafunzi wako?
5. Katika mtaala wa kufundishia,mada ya mofu ipo katika kiwango kulingana na kiwango cha wanafunzi?
6. Uwezo wa uchambuzi wa matumizi wa mofu nafsi na njeo wakati wa ufundishaji upo katika kiwango gani?

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| a. kikubwa | [ ] | b. wastani | [ ] | c.kidogo | [ ] |
| d. kidogo sana | [] | | | | |

7. Toa changamoto za ufundishaji mada ya mofu **nafsi** na **njeo** za Kiswahili.

1 nakubali 2 sikubali 3 sina uhakika

| Na. | Changamoto za ufundishaji wa mada ya mofu nafsi na njeo za Kiswahili Sanifu | 1 | 2 | 3 |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Uhaba wa vitabu vya kufundishia Kiswahili mashuleni | | | |
| 2 | Somo la Kiswahili hupangiwa mwalimu wasio wataalamu | | | |
| 3 | Idadi kubwa ya wanafunzi madarasani | | | |
| 4 | Baadhi ya waalimu kutokuwa na uwelewa mzuri wa mada ya mofu. | | | |
| 5 | Utoro wa wanafunzi katika madarasa | | | |

b)Taja changamoto nyengine unazokutana nazo.

AHSANTE KWA USHIRIKIANO WAKO

**Kiambatisho Na. 2: Dodoso la Utafiti**

Muongozo wa hojaji kwa wanafunzi wanaosoma somo la kiswahili shuleza Zanzibar.

Maelezo

Mimi ni mwanafunzi wa shahada ya uzamili (MA KISWAHILI) Chuo Kikuu Huria cha Tanzania. Hojaji hii madhumuni yake ni kukusanya data za kupima uelewa wa mofu **nafsi** na **njeo** za Kiswahili kwa  za Zanzibar.Taarifa zitakazokusanywa ni kwaajili ya taaluma tu, na majibu yako yatakuwa ni siri na yatatunzwa. Tafadhali jibu maswali yafuatayo kwa ufasaha ili tuweze kukamilisha kazi yetu.

**SEHEMU A: MAELEZO BINAFSI**

Shule …………………………………………………

Tafadhali jaza maelezo katika sehemu zilizowachwa wazi

1. Umri wa mtafitiwa…………………

2. Jinsia ……………………kiwango cha elimu………………………

**SEHEMU B: MAELEZO KUHUSU MADA HUSIKA**

Tafadhali jibu maswali yafuatayo ili tufanikishe kazi yetu.

1.Ushawahi kujifunza mada inayohusiana na mofu nafsi na njeo za Kiswahili?

(weka alama ya vema panapohusika)

Ndio [ ], hapana [ ]

2.Eleza kwa ufupi dhana ya mofu na mofimu

Mofu ………………………………………………………………………..

Mofimu ……………………………………………………………………..

3. Vitenzi vilivyoorodheshwa hapo chini ni vya Kiswahili Sanifu, tafadhali chambuaa) mofu **nafsi**na b) mofu**njeo** katika vitenzi hivyo.

   a) Chambua mofu nafsi :

Mfano;**anacheza** (a) ni nafsi ya tatu umoja,

Ninakwenda……………….…………………………………………………...

Mtaimba………………………………………………………………………..

Unaimba ……………………………………………………………………

Tunakwenda……………………………………………………………………….

Watalia…………………………………………………………………………..

Alilia…………………………………………………………………………….

   a) Chambua mofu njeo:

Mfano;**wataandika** (ta) njeo ya wakati ujao

Ninakwenda……………….…………………………………………………

Mtaimba………………………………………………………………………

Unaimba………………………………………………………………………

Tunakwenda………………………………………………………………….

Watalia…………………………………………………………………………..

Alilia……………………………………………………………………………….

4. Kuna viambishi vingapi vinavyowakilisha:

   a) Mofu **nafsi** b) Mofu**njeo**katika vitenzi vya Kiswahili Sanifu.

   (Weka alama ya vema katika pahala panapohusika)

i) Vitatu [ ] ii) Vinne [ ] iii) Vitano [ ]

iv) Hamna [ ]

**5.** Andika vitenzi vitatu ukiainisha ndani yake mofu **nafsi** na **njeo**

Mfano: anasoma (a) nafsi ya tatu umoja, (na) njeo ya wakati unaoendelea

……………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………….

……………………………………………………………………………………

6. Zifuatazo ni changamoto wakati wa kujifunza mada ya mofu **nafsi** na **njeo**.Weka alama ya vyema unapopahitaji.

1=nakubali 2 =sikubali 3=sina uhakika

| **Na.** | **Changamoto za ujifunzaji wa mada ya mofu nafsi na njeo Kiswahili Sanifu** | **1** | **2** | **3** |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Uhaba wa vitabu vya kujifunzia kiswahili mashuleni. | | | |
| 2 | Muamko mdogo kuhusu somo la kiswahili kwa wanafunzi | | | |
| 3 | Wanafunzi kushindwa kuelewa aina za maneno | | | |
| 4 | Wanafunzi kushinda kutofautisha kati ya mofu na mofimu. | | | |
| 5 | Ugumu wa mada kulingana na kiwango cha wanafunzi | | | |

(b) Zitajechangamoto nyengine unazokumbana nazo.

……………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………

AHSANTE KWA USHIRIKIANO WAKO